# UCHUMI WETU

TOLEO NA. 05, JULAI 2026

BENKI KUU YA TANZANIA
1966-2026

## MIAKA 60 YA BENKI KUU YA TANZANIA: UCHUMI IMARA NA ENDELEVU



# NENO LA GAVANA



**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

Ninayo furaha kukukaribisha katika toleo la tano la jarida hili. Toleo hili ni maalumu kwa kuwa linaangazia kwa kina maadhimisho ya miaka 60 tangu kuanzishwa kwa Benki Kuu ya Tanzania.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) huchapisha Jarida la UCHUMI WETU kila robo mwaka kwa lengo la kuwafikishia wadau wake taarifa, elimu na uelewa kuhusu masuala ya uchumi, sera ya fedha, pamoja na shughuli mbalimbali inazozitekeleza katika kutimiza wajibu wake wa msingi.

Katika kipindi cha miongo sita iliyopita, Benki Kuu imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa weledi, uwajibikaji na uzalendo mkubwa katika kusimamia sera ya fedha, kudhibiti mfumuko wa bei, kuimarisha sekta ya fedha, kusimamia mifumo ya malipo, kutunza akiba ya Taifa pamoja na kuhakikisha mfumo wa fedha unabaki kuwa salama, thabiti na wenye kuhimili misukosuko ya ndani na nje ya nchi. Mafanikio haya yameiwezesha Tanzania kujenga msingi imara wa ukuaji wa uchumi unaowanufaisha wananchi na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na maendeleo endelevu.

Kwa namna ya pekee, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi wake mahiri na maelekezo yake thabiti yanayoendelea kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Maelekezo hayo yameendelea kuwa dira muhimu katika utekelezaji wa sera na mipango mbalimbali inayolenga kuongeza tija ya uchumi, kukuza uwekezaji, kuimarisha sekta ya fedha na kuboresha ustawi wa Watanzania. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kushiriki nasi kwenye sherehe ya maadhimisho ya miaka 60 ya Benki Kuu kama Mgeni Rasmi. Ujio wake ulitupa heshima kubwa na ulidhihirisha imani yake juu ya taasisi yetu kama chombo muhimu katika mustakabali wa uimara wa uchumi wetu.

Vilevile, ninawashukuru Watanzania wote kwa kuendelea kuiamini Benki Kuu ya Tanzania katika kipindi chote cha miaka 60. Imani, ushirikiano na uungwaji mkono mliotupatia vimekuwa nguzo muhimu zinazotuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi na kuendelea kulinda uthabiti wa uchumi wa Taifa letu.

Pamoja na shamrashamra za maadhimisho ya miaka 60 ya Benki Kuu ya Tanzania yaliyobebwa na kaulimbiu isemayo, "Miaka 60 ya Benki Kuu ya Tanzania; Uchumi Imara na Endelevu," shughuli za kawaida za Benki ziliendelea kutekelezwa kwa ufanisi.

Napenda pia kutumia nafasi hii kuwashukuru wageni wote wa ndani na nje ya nchi walioshiriki na kufanikisha maadhimisho ya miaka 60 ya Benki Kuu ya Tanzania. Ushiriki wao umeonesha heshima kubwa waliyonayo kwa taasisi yetu na umedhihirisha mchango wa Benki Kuu katika maendeleo ya uchumi wa Tanzania na ukanda wa Afrika kwa ujumla.

Katika upande wa mwenendo wa uchumi, kasi yake kidunia ilipungua katika robo mwaka iliyoishia Juni 2026, kutokana na kuongezeka kwa athari za mgogoro wa Mashariki ya Kati, ambao ulivuruga usambazaji wa mafuta na njia kuu za biashara. Mgogoro huu ulichangia ongezeko la bei za mafuta ghafi, mbolea, na gharama za usafirishaji. Mwenendo huu umesababisha mfumuko wa bei duniani kuanza kuongezeka na hivyo kudhoofisha matarajio ya ukuaji wa uchumi wa dunia kwa mwaka 2026. Mwelekeo wa uchumi wa dunia utategemea namna mgogoro wa Mashariki ya Kati utakavyoendelea kushughulikuwa na kumalizika.

Pamoja na changamoto zilizotokana na mgogoro wa Mashariki ya Kati, tunashukuru kwamba mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu umeendelea kuwa mzuri. Kwa Tanzania Bara, uchumi unakadiriwa kukua kwa asilimia 6 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2026, ukichangiwa zaidi na ongezeko la uzalishaji katika shughuli za kilimo, ujenzi, madini, huduma za kifedha pamoja na usafirishaji. Uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa asilimia 6.6, ukichochewa zaidi na shughuli za utalii na ujenzi. Katika nusu ya pili ya mwaka 2026, uchumi unatarajiwa kuendelea kuwa imara, ukikua kwa zaidi ya asilimia 6.

Mfumuko wa bei umeendelea kuwa mdogo, licha ya kuongezeka kutokana na kupanda kwa bei za mafuta na gharama za usafirishaji duniani. Kwa upande wa Tanzania Bara, mfumuko wa bei uliongezeka hadi asilimia 4.2 mwezi Mei 2026, kutoka asilimia 3.2 mwezi Machi 2026, ila uliendelea kubaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Aidha, ruzuku ya mafuta iliyotolewa na Serikali mwezi Mei na Juni 2026 ilisaidia kupunguza kasi ya ongezeko la mfumuko wa bei. Kwa upande wa Zanzibar, mfumuko wa bei uliongezeka hadi asilimia 5.5 mwezi Mei 2026 kutoka asilimia 4.9 mwezi Machi 2026, ikilinganishwa na lengo la asilimia 5. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya lengo, licha ya changamoto zilizopo.

Hali ya ukwasi katika robo ya pili ya mwaka 2026 ilikuwa sanjari na mwelekeo wa sera ya fedha. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa kasi ya kuridhisha ya wastani wa asilimia 24, ikichangiwa na ongezeko la mahitaji kutoka katika sekta za uzalishaji. Sekta ya kibenki iliendelea kutengeneza faida, ikiwa na mtaji wa kutosha kukabiliana na misukosuko ya muda mfupi. Aidha, ubora wa rasilimali uliendelea kuwa thabiti, kama inavyodhihirishwa na uwiano wa mikopo chechefu uliokuwa asilimia 2.9 mwezi Mei 2026, ikilinganishwa na kiwango kinachohimilika cha asilimia 5. Wakati huohuo, mifumo ya malipo iliendelea kufanya kazi kwa ufanisi na usalama, jambo linalowezesha uendeshaji wa shughuli za kiuchumi.

Naamini kwamba Jarida hili litakupa habari na taarifa mbalimbali muhimu, na naamini utaendelea kuwa mdau wetu muhimu.

Nakutakia usomaji mwema.

**Emmanuel Mpawe Tutuba**
Gavana
Benki Kuu ya Tanzania

# KUTOKA MEZA YA MHARIRI MKUU

**Ndugu Msomaji,**

Napenda kukukaribisha tena kusoma Jarida la UCHUMI WETU, ambalo kama ilivyo desturi yetu, limesheheni makala, habari na taarifa mbalimbali kuhusu shughuli na mafanikio ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) katika kipindi cha robo mwaka uliopita. Pia nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kuwa nasi katika mwaka wa fedha ulioisha wa 2025/2026 na ninakutakia heri katika mwaka huu mpya wa fedha wa 2026/2027.

Toleo hili ni maalumu kwa kuwa linaangazia kwa kina maadhimisho ya miaka 60 ya Benki Kuu ya Tanzania. Ndani yake utapata historia ya kuanzishwa kwa Benki, sheria zilizoiongoza katika hatua mbalimbali za maendeleo yake, majukumu yake ya msingi, muundo wa kurugenzi zake, pamoja na mafanikio makubwa iliyoyapata katika kipindi cha miongo sita ya uwepo wake.

Miongoni mwa maudhui muhimu tuliyokuandalia ni mahojiano maalumu na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Mpawe Tutuba, ambae anaelezea kwa kina safari yake ya uongozi, mafanikio yaliyopatikana, changamoto alizokutana nazo na matarajio yake kwa Benki Kuu. Vilevile, tumefanya mahojiano na Gavana Mstaafu wa Benki Kuu, Profesa Florens Luoga, ambaye ameeleza uzoefu na mtazamo wake kuhusu maendeleo ya sekta ya fedha nchini.

Kupitia ushirikiano wetu na wadau mbalimbali wa sekta ya fedha, utapata pia fursa ya kusoma habari na makala kutoka taasisi muhimu zikiwemo, Bodi ya Bima ya Amana (DIB) na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), ambazo zinaelezea nafasi yao katika kuimarisha uthabiti wa sekta ya fedha nchini.

Katika kuadhimisha miaka 60 ya Benki Kuu ya Tanzania, ambayo kilele chake kilifanyika tarehe 12 Juni 2026, matawi yote ya Benki nchini yaliendeleza utamaduni wa kurejesha kwa jamii kwa kutoa misaada mbalimbali ikiwemo vitabu, madawati, bima za afya, vifaa vya matibabu, pamoja na kushiriki shughuli za kijamii kwa kushiriki chakula na makundi maalumu. Huu ni uthibitisho wa dhamira ya Benki ya kuendelea kuimarisha uhusiano wake na jamii inayoihudumia.

Aidha, kwa namna ya pekee pia utapata kufahamu maagizo ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa wakati wa kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya BoT ambapo alipata heshima ya kuwa mgeni rasmi.

Ni matumaini yangu kuwa kupitia toleo hili utaendelea kujenga uelewa mpana kuhusu masuala ya uchumi na fedha kupitia makala, habari, mahojiano, vibonzo, shairi, picha na maudhui mengine mbalimbali tuliyokuandalia.

Tunathamini maoni, ushauri na mapendekezo yako. Tafadhali wasiliana nasi kupitia barua pepe: ***botcommunications@bot.go.tz.***

Nakutakia usomaji mwema.



*Victoria Msina*
Meneja Mawasiliano
Benki Kuu ya Tanzania

# BOT YATIMIZA MIAKA 60, YAENDELEA KUWA NGUZO YA UCHUMI WA TANZANIA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akizungumza katika hafla ya maadhimisho ya miaka 60 ya Benki Kuu iliyofanyika JNICC jijini Dar es Salaam tarehe 12 Juni 2026.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeendelea kuwa nguzo muhimu ya uhuru wa kiuchumi wa Tanzania tangu kuanzishwa kwake mwaka 1966, ikihakikisha uthabiti wa bei, uimara wa sekta ya fedha, na maendeleo ya mifumo ya malipo nchini.

Akizungumza katika hafla ya maadhimisho ya miaka 60 ya Benki Kuu iliyofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 12 Juni 2026, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, alisema mafanikio hayo yanaakisi mchango mkubwa wa taasisi hiyo katika kulindda na kuendeleza uchumi wa taifa kwa miongo sita.

Rais Samia alikumbusha kuwa utoaji wa noti za kwanza mwaka 1966, zenye sura ya Mwalimu Julius Nyerere na picha ya Mlima Kilimanjaro, ulikuwa ishara ya kujitegemea kwa taifa na uwezo wake wa kujenga mustakabali wake wa kiuchumi.

Aidha, alieleza kuwa kwa sasa majukumu ya Benki Kuu yamepanuka zaidi na kugusa maisha ya kila siku ya wananchi, wakiwemo walimu, wafanyabiashara wadogo na vijana wajasiriamali, ambao wanategemea uthabiti wa sekta ya fedha katika kufanikisha malengo yao.

Rais Samia alibainisha kuwa katika historia yake, Benki Kuu imeendelea kujibadilisha kulingana na mahitaji ya uchumi, kuanzia kipindi cha Azimio la Arusha, changamoto za kiuchumi za miaka ya 1980, hadi mageuzi ya mfumo wa soko huria, hatua ambazo zimechangia uthabiti wa uchumi wa sasa.

Katika hatua nyingine, aliipongeza Benki Kuu kwa mchango wake katika kukabiliana na changamoto za hivi karibuni, ikiwemo janga la UVIKO-19 pamoja na kupanda kwa bei za bidhaa duniani, akisema hatua zilizochukuliwa zilisaidia kulinda uchumi wa nchi.

Pia aliupongeza Mpango wa Ununuzi wa Dhahabu ya Ndani ulioanzishwa mwaka 2024, ambao umeiwezesha Benki Kuu kununua zaidi ya tani 25 za dhahabu hadi kufikia Mei 2026, na hivyo kuimarisha akiba ya fedha za kigeni.

Akizungumzia mustakabali wa sekta ya fedha, Rais Samia alisisitiza umuhimu wa ubunifu, mageuzi ya kidijitali na ujumuishi wa kifedha, akitaka huduma za kifedha kuwafikia wananchi wote, hususan wanawake, vijana na watu wa vijijini.

Alitoa wito kwa Benki Kuu kushirikiana na Wizara ya Fedha pamoja na wadau wengine kuboresha upatikanaji wa mikopo, kuanzisha mifumo mbadala ya dhamana, na kuweka mazingira wezeshi kwa teknolojia za kifedha na benki za kidijitali.

Aidha, alihimiza kuendelea kupunguza matumizi ya fedha taslimu kwa kuimarisha mifumo ya malipo ya kidijitali, ili kuongeza uwazi na ufanisi katika uchumi.

Kuhusu mabadiliko ya tabianchi, Rais Samia alitaka Benki Kuu kuzingatia athari zake katika sera na usimamizi wa sekta ya fedha, akibainisha kuwa zinaathiri moja kwa moja uzalishaji na uthabiti wa uchumi.

Akihitimisha, Rais Dkt. Samia alisisitiza kuwa katika kufikia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2050, Benki Kuu ina jukumu muhimu la kuhakikisha uthabiti wa bei, uimara wa sekta ya fedha na maendeleo ya masoko ya kifedha kwa ustawi wa taifa.



Gavana Emmanuel Tutuba, akizungumza katika hafla ya maadhimisho ya miaka 60 ya Benki Kuu iliyofanyika JNICC jijini Dar es Salaam tarehe 12 Juni 2026.

Kwa upande wake, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, alisema kuwa katika kipindi cha miaka 25 iliyopita, uchumi wa Tanzania umekua kwa wastani wa asilimia 6.2, kiwango kinachozidi wastani wa asilimia 4.4 kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Aliongeza kuwa mfumuko wa bei umeendelea kudhibitiwa katika kiwango cha tarakimu moja, ukiwa na wastani wa asilimia 7.5 katika kipindi hicho. Hata hivyo, katika miaka mitatu iliyopita, hali imeimarika zaidi ambapo wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.5, ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 3 hadi 5.

Gavana Tutuba alibainisha kuwa mafanikio hayo ni makubwa ikilinganishwa na kiwango cha juu cha mfumuko wa bei cha asilimia 35.3 kilichorekodiwa mwaka 1994, akisisitiza kuwa hatua zilizochukuliwa zimechangia kwa kiasi kikubwa katika kuimarisha uthabiti wa uchumi wa nchi.

Hafla hiyo, iliyokwenda sambamba na uzinduzi wa kitabu maalum cha maadhimisho ya miaka 60 ya BoT, ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kitaifa na kimataifa, wakiwemo Magavana wa Benki Kuu kutoka nchi za EAC na SADC.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akionesha kitabu maalum cha historia ya noti alichokabidhiwa na Gavana Emmanuel Tutuba katika hafla ya maadhimisho ya miaka 60 ya Benki Kuu iliyofanyika JNICC jijini Dar es Salaam tarehe 12 Juni 2026.

# RAIS SAMIA:
# SEKTA YA FEDHA IWE INJINI YA UKUAJI WA UCHUMI




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameagiza sekta ya fedha nchini kupunguza gharama za mikopo, kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha na kuimarisha ushindani ili kuchochea ukuaji wa sekta binafsi.

Rais Samia alitoa maelekezo hayo Juni 12, 2026 jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya miaka 60 ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ambapo alikuwa mgeni rasmi.

Rais Samia alisema mafanikio ya sekta ya fedha hayapaswi kupimwa kwa idadi ya watu wanaofikiwa na huduma hizo pekee, bali kwa mchango wake katika kuboresha maisha ya wananchi na kukuza uchumi.

Alisema mfumo wa fedha unapaswa kuwawezesha wanawake, vijana, wakulima na wafanyabiashara wadogo kupata mitaji kwa urahisi ili kuanzisha na kukuza biashara zao.

"Kipimo chetu kisiwe idadi ya watu wanaofikiwa na huduma za kifedha pekee, bali namna huduma hizo zinavyoongeza kipato, kupanua biashara, kuwawezesha wakulima kupata mitaji kwa wakati na kuwasaidia vijana kuanzisha biashara," alisema Rais Samia.

Aidha, aliwataka wadau wa sekta ya fedha kupitia upya gharama zote za mikopo, ikiwemo riba, ada, bima, masharti ya dhamana na muda wa urejeshaji, akisisitiza kuwa maamuzi ya utoaji wa mikopo yasitegemee dhamana za jadi pekee bali pia historia ya biashara, mauzo na uwezo wa mkopaji kurejesha mkopo.

Rais Samia alisema matumizi ya mifumo ya malipo ya kidijitali yanapaswa kupunguza gharama za miamala, kurahisisha shughuli za biashara na kuongeza ujumuishi wa kifedha bila kuongeza mzigo kwa wafanyabiashara.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar alisema Serikali itaendelea kushirikiana na Benki Kuu katika kuimarisha sera, usimamizi na maendeleo ya sekta ya fedha ili iwe kichocheo kikubwa zaidi cha uwekezaji, biashara na ukuaji wa uchumi.

Kwa upande wake, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Emmanuel Tutuba, alisema uchumi wa Tanzania umeendelea kuonesha uimara katika kipindi cha miaka 25 iliyopita, huku ukikua kwa wastani wa asilimia 6.2, kiwango kinachozidi wastani wa asilimia 4.4 wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Alisema mafanikio hayo yametokana na utekelezaji wa sera madhubuti za uchumi mkuu na usimamizi imara wa sekta ya fedha uliofanywa na Benki Kuu kwa kushirikiana na Serikali.

Tutuba alisema pia mfumuko wa bei umeendelea kudhibitiwa katika kiwango cha tarakimu moja kwa wastani wa asilimia 7.5 katika kipindi hicho cha miaka 25, huku hali ikiimarika zaidi katika miaka mitatu iliyopita ambapo wastani wa mfumuko wa bei umeshuka hadi asilimia 3.5, kiwango kilicho ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 3 hadi 5.

Katika hafla hiyo, Rais Samia alitunukiwa tuzo maalumu ya kinara wa mageuzi ya mifumo na huduma jumuishi za kifedha, ikiwa ni kutambua mchango wake katika kuendeleza mageuzi ya sekta ya fedha na kuongeza ujumuishi wa huduma za kifedha nchini.

# BOT INAVYOJIVUNIA MIAKA 60 YA KUJENGA UCHUMI IMARA, ENDELEVU



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akikabidhiwa tuzo na Gavana Emmanuel Tutuba katika hafla ya maadhimisho ya miaka 60 ya Benki Kuu iliyofanyika JNICC jijini Dar es Salaam tarehe 12 Juni 2026.**

'Ni Safari yenye milima, mabonde'. Msemo huo unatosha kuelezea miaka 60 ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) tangu kuanzishwa kwake na kusimamia uchumi wa nchi.

Tangu kuanza kazi rasmi Juni 14, 1966, BoT imeendelea kusimamia sera ya fedha, kulinda uthabiti wa sekta ya fedha na kuendeleza mifumo ya malipo inayochochea ukuaji wa uchumi.

Katika kipindi hicho, taasisi hiyo imekabiliwa na changamoto mbalimbali za ndani na nje ya nchi, kuanzia misukosuko ya uchumi wa dunia, mabadiliko ya teknolojia hadi athari za migogoro ya kimataifa. Hata hivyo, imeendelea kusimama kama nguzo ya utulivu wa uchumi wa Tanzania.

Wakati BoT ikisheherekea miaka 60 tangu kuanzishwa kwake, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Emmanuel Tutuba katika mahojiano maalumu anasema msingi wa mafanikio hayo ni utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Benki Kuu katika uchumi wa Taifa.

"Nikiendeleza mazuri yaliyofanywa na watangulizi wangu, msisitizo wangu umekuwa katika kuimarisha nafasi ya Benki Kuu katika kudumisha uthabiti wa bei, kulinda uthabiti wa sekta ya fedha, kuboresha mfumo wa sera ya fedha na kusaidia ukuaji wa uchumi jumuishi," anasema Gavana Tutuba.

Gavana Tutuba anasema hayo ni sehemu ya mafanikio ambayo BoT imeyapata huku ikijipanga zaidi katika kufanikisha kufikiwa kwa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2050 inayolenga Tanzania kuwa na uchumi wenye thamani ya Dola za Marekani trilioni 1.

**Ulinzi wa thamani ya fedha ya Tanzania**
Mbali na hilo, moja ya majukumu makuu ya BoT ni kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki katika viwango vinavyokubalika ili kulinda thamani ya fedha.

Gavana Tututuba anasema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Tanzania imeendelea kurekodi wastani wa mfumuko wa bei wa asilimia 3.6, kiwango ambacho kimeendelea kubaki ndani ya malengo ya taifa na chini ya viwango vya kikanda.

Kwa mujibu wa Gavana Tutuba, mafanikio hayo hayakupatikana kwa bahati mbaya bali ni matokeo ya utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na usimamizi wa karibu wa mwenendo wa uchumi.

"Katika miezi ya hivi karibuni ya Januari na Februari, wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.3. Hali hii imeipa Benki Kuu nafasi ya kuendelea na sera nafuu ya fedha ili kusaidia kufikiwa kwa ukuaji mkubwa wa uchumi," anasema.

Anasema uthabiti huo umeiwezesha Tanzania kubaki miongoni mwa nchi zenye mazingira mazuri ya uchumi katika ukanda wa Afrika Mashariki, huku ukiwawezesha wananchi kulinda uwezo wao wa kununua bidhaa na huduma.

Mbali na kudhibiti mfumuko wa bei, BoT imeendelea kuweka mazingira yanayochochea ukuaji wa uchumi.

Takwimu zinaonyesha kuwa pato la taifa limekuwa likikua kwa wastani wa asilimia 5.7 katika miaka ya karibuni, huku sekta za kilimo, ujenzi, biashara, madini na huduma za fedha zikiendelea kuwa injini muhimu za ukuaji huo.

Tutuba anasema uwekezaji wa Serikali katika miundombinu pamoja na mazingira bora ya biashara umechangia kwa kiasi kikubwa mafanikio hayo.

"Ukuaji huo umechangiwa na sekta za kilimo, ujenzi, huduma za fedha na bima, biashara pamoja na madini. Maendeleo ya miundombinu na mazingira bora ya biashara nayo yamekuwa nguzo muhimu ya ukuaji huo," anasema.

Gavana Tutuba anaongeza kuwa kwa viashiria vya sasa vinaonyesha Tanzania ipo katika nafasi nzuri ya kuendelea kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

**Sekta thabiti ya benki**
Moja ya maeneo ambayo BoT inayajivunia ni uimara wa sekta ya benki.

Katika miaka ya hivi karibuni, kiwango cha mikopo chechefu kimeendelea kushuka huku benki nyingi zikiendelea kuwa na mtaji wa kutosha na ukwasi wa kuridhisha.
Mkurugenzi wa Usimamizi wa Sekta ya Fedha BoT, Bw. Sadati Musa, anasema sekta ya fedha yenye afya ni msingi muhimu wa maendeleo ya uchumi.

"Sekta ya fedha iliyo imara inaongeza imani kwa wananchi na kuchochea ukuaji wa uchumi wa taifa," anasema katika mahojiano maalumu kuhusu miaka 60 ya BoT.

Bw. Musa anaongeza kuwa matumizi ya teknolojia, maboresho ya mifumo ya usimamizi wa vihatarishi na utekelezaji wa sera bora vimechangia kuimarika kwa sekta hiyo nyeti katika uchumi wan chi.

**Mapinduzi ya kidijitali**

Katika zama ambazo dunia inaelekea kwenye uchumi wa kidijitali, BoT nayo imeendelea kuwekeza katika mifumo ya kisasa ya teknolojia ya fedha ambayo inarahisisha malipo tofauti na ilivyokuwa awali.

Mkurugenzi wa Huduma za Kibenki BoT, Bw. Agathon Kipandula, anasema mageuzi hayo yameongeza tija kwa kiwango kikubwa ndani ya Benki Kuu.

"Mwaka 2010 tulikuwa tunashughulikia miamala 2,000 kwa siku kwa kutumia wafanyakazi 60. Mwaka 2026 tunashughulikia zaidi ya miamala 5,000 kwa siku kwa wafanyakazi 32 pekee," anasema.

Bw. Kipandula anasema kupitia mifumo ya kidijitali ya malipo ya TISS, TACH na TIPS, wananchi sasa wanaweza kufanya miamala kwa haraka, usalama na gharama nafuu.

Kwa upande wake, Gavana Tutuba anasema maendeleo hayo yamechangia pia kuongeza ujumuishaji wa kifedha nchini.

"Tanzania imepiga hatua kubwa katika ujumuishaji wa kifedha kupitia huduma za fedha kwa njia ya simu na mifumo ya malipo ya kidijitali yenye ufanisi. Mafanikio hayo yamechangia kupunguza gharama za miamala, kurahisisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kuongeza uwazi katika matumizi ya fedha," anasema.

**Safari ya kuelekea uchumi jumuishi**
Mbali na kuhakikisha uthabiti wa mfumo wa fedha, BoT imeeleza kuwa imeendelea kupanua upatikanaji wa huduma rasmi za kifedha kwa wananchi.

Mkurugenzi wa Ustawi na Huduma Jumuishi za Fedha BoT, Bw. Kennedy Komba, anasema hatua kubwa zimepigwa katika kuwafikia wananchi wengi zaidi kupitia huduma za kidijitali.

"Mwaka 2023 Watanzania waliokuwa wakifikia huduma rasmi za fedha walikuwa asilimia 89 huku wanaotumia huduma hizo wakifikia asilimia 76. Hii ni hatua kubwa ya ujumuishaji wa kifedha ikilinganishwa na awali ambapo pengine takwimu zilikuwa chini zaidi," anasema.

Kwa mujibu wa Bw. Komba, mifumo ya kidijitali imewapa wananchi uwezo wa kupata elimu ya fedha na kuwasilisha malalamiko bila kulazimika kufika katika ofisi za Benki Kuu.

**Kuangalia miaka ijayo**
Mkurugenzi wa Usimamizi wa Sekta ya Fedha BoT, Bw. Sadati Musa kuhusu mustakabali wa BoT miaka ijayo anasema matumizi ya akili unde, uchambuzi mkubwa wa takwimu na mifumo ya usimamizi wa papo kwa papo ni baadhi ya maeneo ambayo taasisi hiyo imeanza kuyawekea msingi.

Bw. Musa anasema teknolojia hizo zitasaidia kutambua vihatarishi mapema kabla havijawa tishio kwa mfumo wa fedha.

"Tunajenga mfumo wa kisasa utakaotumia teknolojia za Akili Unde (AI), hatua ambayo itasaidia kutambua vihatarishi mapema na kusaidia kuifanya sekta ya fedha kuwa thabiti," anasema.

Kwa upande wa huduma jumuishi za fedha, Bw. Komba anaamini Tanzania inaelekea kufikia hatua ambapo karibu kila mwananchi atakuwa sehemu ya mfumo rasmi wa kifedha.

"Naiona Tanzania ikiwa imefikia zaidi ya asilimia 99 ya wananchi wanaotumia huduma rasmi za fedha kwa urahisi na usalama," anasema.

Kwa upande wake, Gavana Tutuba anasema BoT itaendelea kujenga uchumi wenye ushindani, unaojumuisha wananchi wote na wenye uwezo wa kustahimili misukosuko ya ndani na nje ya nchi.

"Ningependa kuwahakikishia Watanzania kuwa Benki Kuu itaendelea kulinda uthabiti wa bei, kuhakikisha uimara wa mfumo wa fedha na kusaidia ukuaji endelevu na jumuishi wa uchumi sambamba na utekelezaji wa Dira ya Taifa ya 2050," anasisitiza

# BENKI KUU YA TANZANIA TUITAKAYO MIAKA 60 IJAYO



Umewahi kufikiria miaka 60 ijayo dunia itakuwaje? Swali hilo linakuja wakati Benki Kuu ya Tanzania ikiadhimisha kufikisha miaka hiyo tangu kuanzishwa kwake huku tafakuri kuu ikiwa tutakuwa wapi miaka kama hiyo ijayo?

Swali hilo linaibua majibu mbalimbali huku wataalamu na viongozi waandamizi wakiiona BoT yenye mifumo thabiti ya kidijitali, matumizi bora ya akili unde na uchumi usiotegemea fedha taslimu.

Wakizungumza kuhusu mustakabali wa Benki Kuu, viongozi wa taasisi hiyo wanaeleza kuwa Tanzania inaelekea kuwa miongoni mwa nchi zenye mifumo ya fedha ya kisasa zaidi barani Afrika.

**Malipo yatakayojifanyia kazi yenyewe**
Kwa upande wa Huduma za Kibenki, matarajio ni kuona mifumo mingi ya malipo ikifanya kazi kiotomatiki bila kuhitaji uingiliaji mkubwa wa binadamu.

Bw. Agathon Kipandula ambaye ni mkurugenzi wa Huduma za Kibenki anasema BoT itaongeza matumizi ya mfumo wa Uchakataji wa Moja kwa Moja wa Miamala yaani Straight Through Processing (STP).

"Tunatarajia mifumo ya malipo itajipitisha yenyewe, kazi kufanyika kwa saa 24 na gharama za uendeshaji kupungua kwa kiasi kikubwa," anasema.

**Sarafu zenye usalama wa hali ya juu**
Katika Kurugenzi ya Usimamizi wa Sarafu, matarajio ni kuona noti na sarafu zikiwa na viwango vya juu zaidi vya usalama ili kuendana na maendeleo ya teknolojia duniani.

Mkurugenzi anayeshughulikia masuala hayo, Dkt. Nguling'wa Balele anasema Benki Kuu itaendelea kuboresha alama za kiusalama kwenye fedha.

"Tutaendelea kutoa noti na sarafu zenye ubora mkubwa na zinazokidhi mahitaji ya teknolojia ya kisasa," anasema.

**Uchumi unaoendeshwa kwa takwimu za wakati halisi**
Kwa mujibu wa Kurugenzi ya Tafiti na Sera za Uchumi, miaka ijayo Benki Kuu itatumia zaidi mifumo ya uchambuzi wa kisasa na takwimu za wakati halisi katika kufanya maamuzi ya sera.

Mkurugenzi wa Kurugenzi hiyo anasema teknolojia itabadilisha kabisa namna sera za fedha zinavyotungwa.

"Benki Kuu itaendelea kuwa taasisi imara katika uchambuzi wa uchumi na utungaji wa sera zinazokabiliana na changamoto za dunia," anasema Dkt. Suleiman Missango ambaye ni mkurugenzi wa Tafiti na Sera za Uchumi BoT.

**Zaidi ya asilimia 99 ya Watanzania kufikiwa na huduma za fedha**
Katika Kurugenzi ya Ustawi na Huduma Jumuishi za Fedha, matarajio makubwa ni kuona karibu kila Mtanzania akifikia huduma rasmi za kifedha.

Akizungumzia hilo, mkurugenzi wake, Bw. Kennedy Komba anasema huduma nyingi zitakuwa zinapatikana kidijitali kwa gharama nafuu.

"Naiona Tanzania ikiwa imefikia zaidi ya asilimia 99 ya wananchi wanaotumia huduma rasmi za fedha kwa urahisi na usalama," anasema.
Anaongeza kuwa matumizi ya fedha taslimu yatapungua sana huku elimu ya fedha ikianza kufundishwa kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu.

**AI kusimamia sekta ya fedha**
Kwa upande wa Kurugenzi ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Benki Kuu ya miaka ijayo itaendeshwa zaidi kwa teknolojia za akili bandia na mifumo ya kisasa ya uchambuzi wa vihatarishi.

Mkurugenzi wa Kurugenzi hiyo anasema taasisi hiyo itakuwa na uwezo mkubwa wa kugundua matatizo kabla hayajaathiri mfumo wa fedha.

"Tutakuwa na mfumo wa usimamizi wa papo kwa papo utakaotumia AI, Big Data na Machine Learning katika kusimamia sekta ya fedha," anasema.

**Tanzania kuelekea uchumi usiotumia fedha taslimu**
Kurugenzi ya Mifumo ya Malipo ya Taifa inaona miaka ijayo Tanzania ikiingia zaidi kwenye uchumi wa kidijitali usiotegemea fedha taslimu.

Mkurugenzi wa Mifumo ya Malipo ya Taifa, Bi. Lucy Shahidi anasema mifumo hiyo katika miaka 60 ijayo itaunganishwa kikamilifu ndani na nje ya nchi.

"Benki Kuu itaendelea kuwa kinara wa mageuzi ya kidijitali kwa kuhakikisha mifumo ya malipo inakuwa ya haraka, salama na yenye gharama nafuu," anasema.

Anasema matumizi ya teknolojia kama akili bandia, uchambuzi mkubwa wa takwimu na hata sarafu za kidijitali za Benki Kuu (CBDC) yataongeza ufanisi wa huduma za kifedha nchini.

Kwa ujumla, taswira ya Benki Kuu katika miaka 60 ijayo ni ya taasisi ya kisasa zaidi, inayotumia teknolojia kuimarisha uchumi, kuongeza ujumuishi wa kifedha na kuwahudumia wananchi kwa kasi, usalama na uwazi mkubwa zaidi.

# SADC-CCBG YAKUTANA DAR WAKATI BOT IKIADHIMISHA MIAKA 60





Gavana Emmanuel Tutuba akizungumza katika akizungumza katika Mkutano wa 62 wa Kamati ya  Magavana wa Benki Kuu za Jumuiya ya SADC, uliofanyika tarehe 11 Juni 2026 katika hoteli ya Serena.




Washiriki  wakifuatilia mkutano wa Kamati ya Magavana wa Benki Kuu za jumuiya ya SADC (SADC CCBG) uliofanyika tarehe 11 Juni 2026 katika hoteli ya Serena




Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeadhimisha miaka 60 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1966, tukio lenye uzito mkubwa katika historia ya sekta ya fedha nchini. Maadhimisho hayo yamepambwa na matukio mbalimbali muhimu, ikiwemo kufanyika kwa Mkutano wa 62 wa Kamati ya Magavana wa Benki Kuu za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC-CCBG), uliofanyika tarehe 11 Juni 2026 katika Hoteli ya Serena jijini Dar es Salaam.

Akifungua rasmi mkutano huo, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw.Emmanuel Tutuba, aliwakaribisha wageni kutoka nchi mbalimbali na kueleza furaha yake kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huo unaowakutanisha viongozi wakuu wa sekta ya fedha katika ukanda wa SADC. Alibainisha kuwa uwepo wa mkutano huo wakati wa maadhimisho ya miaka 60 umeongeza umuhimu na hadhi ya tukio hilo.

Katika hotuba yake ya ukaribisho, Gavana Tutuba aliangazia changamoto za kiuchumi zinazoikabili kanda ya SADC, akitaja hasa athari za migogoro inayoendelea Mashariki ya Kati. Alieleza kuwa hali hiyo imeongeza ugumu wa mazingira ya kiuchumi na kusisitiza kuwa mkutano huo ni fursa muhimu kwa nchi wanachama kujadili na kuoanisha mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo.

Akizungumzia hali ya uchumi wa Tanzania, alisema kuwa nchi imeendelea kuonyesha uimara licha ya changamoto za kimataifa. Alifafanua kuwa uchumi ulikua kwa asilimia 5.9 mwaka 2025 na unatarajiwa kufikia asilimia 6.3 mwaka 2026. Hata hivyo, alionya kuwa mfumuko wa bei umeanza kuongezeka kidogo katika miezi ya hivi karibuni, ingawa bado uko ndani ya kiwango kilicholengwa cha asilimia 3 hadi 5.

Akihitimisha hotuba yake, Gavana Tutuba aliwahimiza wageni kufurahia vivutio mbalimbali vya utalii vilivyopo nchini Tanzania, ikiwemo jiji la Dar es Salaam pamoja na Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, ambako ziara maalum imepangwa kufanyika. Vilevile aliwataka wageni watakaopata muda kutembelea maeneo maarufu kama Zanzibar, Serengeti, Mlima Kilimanjaro na Bonde la Ngorongoro ili kujionea vivutio vya kipekee na kubeba kumbukumbu nzuri ya ziara yao nchini.

# BONANZA LA MAADHIMISHO YA MIAKA 60 YA BOT LAFANA

Ikiwa ni mfululizo wa matukio kipindi cha maadhimisho ya miaka 60 ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) yaliyofanyika Juni 12, 2026 jijini Dar es Salaam, shughuli mbalimbali zilifanywa ikiwamo bonanza.

Bonanza hilo lilifanyika tarehe Juni 6, 2026 katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam na kuwashirikisha wafanyakazi wa Benki Kuu pamoja na wadau mbalimbali.

Akizungumza wakati wa Bonanza hilo, Mgeni Rasmi ambaye pia ni Naibu Gavana wa BoT anayesimamia Uthabiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Bi. Sauda Msemo, alisema kuwa michezo ni nyenzo muhimu ya kuimarisha afya, mshikamano na ushirikiano miongoni mwa wafanyakazi.

Alieleza kuwa mshikamano unaojengwa kupitia matukio ya michezo huchangia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi, jambo ambalo lina mchango mkubwa katika kukuza na kustawisha uchumi wa nchi.










# MAHOJIANO GAVANA WA BoT: ILIKOTOKA, ILIPO NA INAPOENDA



Ni miaka 60 tangu kuanzishwa kwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT). Ingalikuwa ni mtumishi wa umma kwa umri huo angalikuwa tayari kustaafu rasmi serikalini, ama kwa hakika ni kipindi kirefu.

Safu hii imepata bahati ya kufanya mahojiano na Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba kuangazia ndani ya kipindi hicho mafanikio na changamoto katika safari ya miaka hiyo lakini pia kufahamu yapi malengo ya taasisi hiyo nyeti kwa miaka ijayo.

**Swali: Ulipoteuliwa kuongoza Benki Kuu Januari 2023, uliweka vipaumbele vipi na mpaka sasa unajivunia vitu gani katika usimamizi wa uchumi wa Tanzania?**

**Jibu:** Nikiendeleza mazuri yaliyofanywa na watangulizi wangu msisitizo wangu umekuwa katika kuimarisha nafasi ya Benki Kuu katika kudumisha uthabiti wa bei, kulinda uthabiti wa sekta ya fedha, kuboresha mfumo wa sera ya fedha na kusaidia ukuaji wa uchumi jumuishi.

Sera ya fedha imeendelea kulenga kudhibiti mfumuko wa bei ndani ya kiwango kinacholengwa cha asilimia 3 hadi 5 sambamba na kuwezesha ukuaji wa uchumi. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.6, sambamba na viwango vya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) vya asilimia 8 na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) vya asilimia 3 hadi 7. Katika miezi ya hivi karibuni ya Januari na Februari, wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.3.

Mafanikio hayo yametokana na athari za muda za sera ya fedha, kupungua kwa athari za mabadiliko ya viwango vya ubadilishaji fedha na kushuka kwa mfumuko wa bei wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje, hasa bidhaa za mafuta. Hali hii imeipa Benki Kuu nafasi ya kuendelea na sera nafuu ya fedha ili kusaidia kufikiwa kwa ukuaji mkubwa wa uchumi.

Pato la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 5.7 kati ya mwaka 2017 hadi 2024, huku kati ya mwaka 2021 hadi 2024 nchi ikirekodi wastani wa ukuaji wa asilimia 5.2, kiwango kilichozidi wastani wa asilimia 4.0 wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Sekta zilizochangia ukuaji huo ni pamoja na kilimo, ujenzi, huduma za fedha na bima, biashara na ukarabati pamoja na madini.

Ukuaji wa sekta ya kilimo umechochewa na uwekezaji unaoendelea, hususan katika miradi ya umwagiliaji, pamoja na usambazaji wa mbolea, mbegu na viuatilifu kwa wakati. Aidha, uwekezaji wa Serikali katika miradi mikubwa ya miundombinu ikiwemo reli, barabara, viwanja vya michezo na viwanja vya ndege umeendelea kuchochea shughuli za kiuchumi. Maendeleo hayo pia yameimarishwa na mazingira bora ya biashara, sera thabiti za uchumi jumla pamoja na uwezo wa kukabiliana na misukosuko ya nje.

Kwa mtazamo wa baadaye, uchumi unatarajiwa kuendelea kukua kwa zaidi ya asilimia 5 kuelekea lengo la ukuaji wa zaidi ya asilimia 10 lililowekwa katika Dira ya Taifa ya 2050. Ukuaji huo utachangiwa na maendeleo ya miundombinu, ongezeko la tija katika kilimo, kuongezeka kwa uzalishaji wa madini, matumizi ya teknolojia pamoja na kuimarika kwa sekta ya viwanda. Viashiria vya sasa vinaonesha kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi, ukuaji wa mauzo ya nje, ongezeko la uzalishaji wa umeme, uzalishaji wa bidhaa za viwandani ikiwemo saruji pamoja na kuimarika kwa sekta ya utalii.

**Swali: Katika kipindi chako cha uongozi, Benki Kuu imefanya mageuzi mbalimbali ya kisera na kiusimamizi katika sekta ya fedha. Ni kwa namna gani hatua hizo zimechangia kuimarika kwa uthabiti wa sekta ya benki?**

**Jibu:** Katika kuimarisha ustahimilivu wa sekta ya fedha, Benki imeendelea kuboresha usimamizi wa sekta ya benki, kuimarisha mifumo ya usimamizi wa vihatarishi na kulinda uthabiti wa mfumo wa fedha. Ripoti za hivi karibuni zinaonesha kupungua kwa mikopo chechefu, kuimarika kwa ukwasi na kuongezeka kwa faida za benki kutokana na upanuzi wa huduma za uwakala wa benki pamoja na mageuzi ya kimuundo.

Viashiria vyote vya sekta ya fedha vinaendelea kubaki ndani ya viwango vinavyokubalika kutokana na kuimarishwa kwa usimamizi wa vihatarishi, matumizi ya teknolojia, uimara wa mtaji na maboresho ya sera. Sekta ya benki ambayo inachangia takribani asilimia 70 ya sekta ya fedha ina mtaji wa kutosha, ukwasi wa kuridhisha na inaendelea kupata faida huku ikitumia teknolojia katika utoaji wa huduma. Kufikia Desemba 2025, Tanzania ilikuwa na benki 42 zenye mtandao wa matawi 1,046.

Benki zimeendelea kuwa na mtaji wa kutosha wa kukabiliana na misukosuko mbalimbali, huku kiwango cha Common Equity Tier I kikiwa asilimia 19.3 Januari 2026, zaidi ya kiwango cha chini kinachotakiwa cha asilimia 10. Uwiano wa mali ukwasi dhidi ya madeni ya muda mfupi ulikuwa asilimia 26.51 Februari 2026, juu ya kiwango cha chini kinachotakiwa cha asilimia 20. Ubora wa mali za benki pia umeimarika ambapo kiwango cha mikopo chechefu kilifikia asilimia 2.9 mwishoni mwa Februari 2026, ndani ya kiwango kinachokubalika cha asilimia 5, kutoka asilimia 8.7 mwaka 2015/16.

Katika kukuza ujumuishaji wa kifedha na ubunifu, Benki imeendelea kupanua upatikanaji wa huduma za kifedha na kusaidia ubunifu katika mifumo ya malipo ikiwemo maendeleo ya miundombinu ya kisasa ya malipo ya kidijitali. Hatua hizo zimekuwa kichocheo cha ukuaji wa sekta ya fedha, kupunguza umasikini na kuimarisha uthabiti wa mfumo wa fedha.

Mwaka 2025, Kiashiria cha Ujumuishaji wa Kifedha Tanzania (TanFiX) kiliongezeka hadi 0.83 kutoka 0.72 mwaka 2023, jambo linaloonesha kuongezeka kwa vituo vya huduma, matumizi ya huduma za kifedha za kidijitali, elimu ya fedha pamoja na mfumo mzuri wa udhibiti. Sekta ndogo ya huduma ndogo za fedha pia imeendelea kuimarika kupitia usimamizi wa wakopeshaji wa kidijitali na utoaji wa leseni kwa watoa huduma wapya.

Katika kuendeleza ubunifu, Benki ilizindua mfumo wa majaribio wa

Fintech Regulatory Sandbox baada ya kutungwa kwa Kanuni za Fintech Regulatory Sandbox mwaka 2024, hatua inayowezesha majaribio ya suluhisho za kifedha zinazotumia teknolojia mpya katika mazingira salama na yanayodhibitiwa.

Aidha, Benki imeendelea kuwekeza katika rasilimali watu ili kuhakikisha taasisi inaendelea kuwa yenye kuaminika, yenye mtazamo wa mbele na yenye uwezo wa kukabiliana na changamoto zinazojitokeza.

Kuhusu maamuzi ya kisera, moja ya maamuzi muhimu zaidi katika kipindi changu cha uongozi ni mabadiliko ya mfumo wa sera ya fedha kutoka ule wa udhibiti wa kiwango cha fedha kwenda mfumo unaotumia viwango vya riba, hatua iliyoiweka Tanzania sambamba na mifumo ya kisasa ya benki kuu duniani.

**Swali: Januari 2024, Benki ilihama rasmi kutoka mfumo wa ujazi wa fedha kwenda mfumo wa sera ya fedha unaotegemea viwango vya riba. Kwa nini mabadiliko hayo yalionekana kuwa muhimu?**

**Jibu:** Benki Kuu ya Tanzania ilihamia rasmi katika mfumo wa sera ya fedha unaotegemea viwango vya riba Januari 2024, baada ya kutumia kwa miaka 28 mfumo unaotegemea ujazi wa fedha. Katika mfumo huo mpya, Benki hutumia kiwango cha riba cha Benki Kuu, ambacho kwa sasa ni asilimia 5.75, kuelekeza viwango vya riba katika soko la benki kwa lengo la kudhibiti mfumuko wa bei na kuendana na viwango vya kimataifa.

Mabadiliko hayo yalifanyika kwa sababu mfumo wa viwango vya riba unawezesha maamuzi ya sera ya fedha kufika kwa ufanisi zaidi katika uchumi kupitia viwango vya riba vya muda mfupi. Aidha, ubunifu wa kifedha na mabadiliko ya mazingira ya kifedha yalikuwa yamepunguza ufanisi wa mfumo wa zamani wa kulenga kiasi cha fedha.

Mfumo mpya pia umeongeza uwazi na mawasiliano kwa masoko na umma kuhusu mwelekeo wa sera ya fedha ya Benki. Vilevile, mabadiliko hayo yalichangiwa na mahitaji ya kikanda chini ya mchakato wa Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki pamoja na kuendana na mwenendo wa benki kuu nyingi duniani ambazo zimehamia katika mifumo hiyo kadri masoko ya fedha yanavyoendelea kukua na kuwa ya kisasa zaidi.

Hatua hiyo ni muhimu kwa sababu inawezesha udhibiti sahihi zaidi wa mfumuko wa bei, kusaidia uthabiti wa gharama za mikopo na kuongeza uwazi kupitia mawasiliano ya maamuzi ya sera kwa Kamati ya Sera ya Fedha, wakurugenzi wakuu wa benki za biashara pamoja na umma, hivyo kuongeza utabirika kwa wafanyabiashara na wawekezaji.

**Swali: Ukiangalia mbele, unaona changamoto na fursa gani kwa Benki katika kipindi cha miaka kumi ijayo?**

**Jibu:** Benki italazimika kukabiliana na mazingira ya fedha yanayobadilika kwa kasi duniani na ndani ya nchi huku ikitumia vizuri fursa zinazotokana na teknolojia, ubunifu wa kifedha na kuimarika kwa masoko ya fedha.

Miongoni mwa changamoto zilizopo ni pamoja na kuyumba kwa uchumi wa dunia, mwenendo wa siasa za kimataifa pamoja na misukosuko ya nje. Pia ipo changamoto ya kudhibiti mfumuko wa bei kutokana na kupanda kwa bei za mafuta na mabadiliko ya hali ya fedha duniani. Benki pia itaendelea kufuatilia vihatarishi vipya kama mashambulizi ya mtandao, mabadiliko ya teknolojia na bidhaa mpya za kifedha.

Aidha, athari za mabadiliko ya tabianchi kwa uthabiti wa sekta ya fedha na ustahimilivu wa uchumi nazo ni changamoto muhimu.

Kwa upande wa fursa, kuendelea kwa huduma za kifedha za kidijitali ikiwemo huduma za simu za mkononi na mifumo ya malipo ya kielektroniki ni nafasi muhimu ya kuongeza ujumuishaji wa kifedha na kuboresha ufanisi wa miamala ya kifedha nchini.

Pia, maendeleo ya masoko ya fedha na mitaji nchini yatasaidia matumizi bora ya rasilimali za kifedha, kuboresha utekelezaji wa sera ya fedha na kuongeza vyanzo vya fedha kwa Serikali na sekta binafsi. Ushirikiano wa kifedha ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Jangwa la Sahara (SADC) nao utatoa fursa za kuimarisha malipo ya mipakani, kukuza masoko ya fedha na kuongeza ushirikiano wa kiuchumi.

Moja ya nguvu kubwa za Benki katika siku zijazo ni kuendelea kuwekeza katika rasilimali watu. Katika miaka ya hivi karibuni Benki imewekeza kwa kiwango kikubwa katika kujenga wataalamu wenye ujuzi wa hali ya juu katika idara mbalimbali. Hatua hiyo imeongeza uwezo wa uchambuzi, kusaidia utungaji wa sera bora na kuhakikisha Benki inaendelea kuwa tayari kukabiliana na changamoto mpya za uchumi na sekta ya fedha.

**Swali: Benki inapoadhimisha miaka 60, ni ujumbe gani ungependa kuwapa Watanzania?**

**Jibu:** Ningependa kuwahakikishia Watanzania kuwa Benki Kuu itaendelea kulinda uthabiti wa bei, kuhakikisha uimara wa mfumo wa fedha na kusaidia ukuaji endelevu na jumuishi wa uchumi sambamba na utekelezaji wa Dira ya Taifa ya 2050.

Kwa miaka yote, Benki imeendelea kutekeleza wajibu wake wa kudhibiti mfumuko wa bei, kulinda uthabiti wa sekta ya fedha na kukuza maendeleo ya mfumo bora wa fedha. Aidha, Benki imeendelea kushirikiana kwa karibu na Serikali, taasisi za fedha na wadau mbalimbali katika kusaidia mageuzi ya uchumi na maendeleo ya sekta ya fedha.

Kadri Tanzania inavyoendelea kuelekea katika utekelezaji wa malengo ya muda mrefu ya maendeleo yaliyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050, Benki Kuu itaendelea kuwa na nafasi muhimu katika kuhakikisha uthabiti wa uchumi pamoja na kujenga mfumo wa fedha ulio imara na jumuishi.

Benki Kuu pia itaendelea kuimarisha rasilimali watu, kukumbatia ubunifu na kusaidia sera zinazochochea ukuaji endelevu na jumuishi wa uchumi.

Aidha, ningependa kuhamasisha Watanzania kuendelea kutumia huduma za kifedha za kidijitali na mifumo ya malipo ya kielektroniki. Matumizi ya mifumo hiyo yanaongeza urahisi na ufanisi katika miamala ya kila siku, yanasaidia kujenga mfumo wa fedha jumuishi na wenye nguvu, hupunguza gharama za matumizi ya fedha taslimu na kusaidia ufanisi wa utekelezaji wa sera ya fedha.

# BOT YARUDISHA KWA JAMII IKISHEREKEA MIAKA 60 TANGU KUANZISHWA



Benki Kuu ya Tanzania (BoT) katika kuadhimisha Miaka 60 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1966 na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imefanya zoezi la kurudisha kwa jamii (Corporate Social Responsibility-CSR) kwa kufanya usafi katika fukwe ya Dengu iliyopo wilaya ya Ilala, Dar es Salaam.

Tukio hilo lililofanyika tarehe 11 Juni 2026 lilihusisha wafanyakazi wa Benki Kuu,halmashauri ya jiji la Dar es Salaam, kampuni za usafi pamoja na wanafunzi wa shule mbalimbali.

Akizungumza wakati wa shughuli hiyo, Naibu Gavana wa BoT anayesimamia Utawala na Udhibiti wa Ndani, Dkt. Rahma Mahfoudh, alisema kuwa pamoja na mafanikio makubwa ambayo Benki Kuu imeyapata katika kusimamia uchumi wa nchi, inatambua umuhimu wa kurudisha kwa jamii, ikiwemo uhifadhi na utunzaji wa mazingira. "Baada ya kutafakari namna bora ya kuadhimisha miaka 60 ya Benki, tulikubaliana kwamba njia bora zaidi ya kusherehekea mafanikio yetu ni kurejesha sehemu ya mafanikio hayo kwa jamii kupitia shughuli za kuhifadhi mazingira". Alisema Naibu Gavana huyo.

Aliongeza kuwa kwa kutambua umuhimu wa utunzaji mazingira, Benki Kuu pia, imenunua na itakabidhi mapipa ya kuhifadhia taka kwa shule, masoko na maeneo ya mbalimbali ya umma.

"Mapipa haya si vifaa vya kuhifadhia taka pekee. Ni uwekezaji katika utamaduni wa usafi, afya ya jamii na uhifadhi wa mazingira. Tunatarajia yatasaidia kuhamasisha wananchi, wanafunzi na wafanyabiashara kuendelea kutunza mazingira yao kila siku". Alisisitiza.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Bw. Edward Mpogoro, aliipongeza BoT kwa kuendesha shughuli hiyo ya utunzaji wa mazingira na kwa kugawa mapipa ya kutupia taka kwa ajili ya kuimarisha usafi wa mazingira.

Ukiachana na shughuli hiyo kufanyika kitaifa jijini Dar es Salaam, pia katika matawi mbalimbali ya BoT yalirudisha kwa jamii.

**Dodoma washiriki michezo, watoa misaada Mpwawa, Chemba**
Katika Makao Makuu ya BoT Dodoma, maadhimisho yalifanyika katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), yakihusisha michezo na burudani mbalimbali.

Baada ya michezo hiyo, walitoa misaada ya vitabu katika shule za sekondari wilayani Chemba pamoja na vifaa vya hospitalini ikiwemo vitanda na viti mwendo katika Wilaya ya Chemba.

**Arusha yatoa msaada kwa watoto wenye seli mundu**
Kwa upande wa tawi la Arusha, liliadhimisha miaka 60 kwa kugusa maisha ya jamii kupitia sekta ya afya.

Tawi hilo lilitembelea Hospitali ya Mount Meru na kulipia bima za afya kwa watoto 50 wanaoishi na ugonjwa wa seli mundu (sickle cell), hatua iliyolenga kusaidia upatikanaji wa huduma za matibabu kwa watoto hao.

**Mbeya yaandaa mdahalo wa kitaaluma**
Katika Mkoa wa Mbeya, maadhimisho yalianza kwa bonanza la michezo mbalimbali lililowakutanisha wafanyakazi na wadau wa benki hiyo.

Jioni, tawi hilo liliandaa mdahalo wa kitaaluma uliolenga kujadili mchango wa BoT katika ukuaji wa uchumi wa Tanzania, huku washiriki wakipata fursa ya kutafakari mafanikio ya miaka 60 ya usimamizi wa sera za fedha na uthabiti wa sekta ya fedha nchini.

**Mwanza na Chuo cha Benki waelimisha umma**
Tawi la Mwanza kwa kushirikiana na Chuo cha Benki walifanya matembezi ya asubuhi pamoja na kutoa elimu ya fedha kwa makundi mbalimbali ya watumishi wa umma.

Walionufaika na mafunzo hayo ni askari, manesi na walimu wa Mkoa wa Mwanza, ambapo walipatiwa maarifa kuhusu usimamizi wa fedha binafsi, matumizi sahihi ya huduma za kifedha na umuhimu wa kujiwekea akiba.





# MAHOJIANO MAALUMU NA GAVANA MSTAAFU PROFESA LUOGA : ASIVYOUSAHAU UVIKO-19



Wakati Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ikiadhimisha miaka 60 ya kuanzishwa kwake, zipo nyakati na watu ambao huwezi kuwasahau.

Katika safu hii, tumefanya mahojiano maalumu na Gavana Mstaafu wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Prof. Florens Luoga, ambaye ameeleza safari ya maendeleo ya Benki Kuu tangu kuanzishwa kwake, mchango wa magavana waliopita, mafanikio yaliyopatikana pamoja na changamoto enzi za uongozi wake.

Kati ya yote 'aliyofunguka' Prof. Luoga kipekee anasema miongoni mwa changamoto iliyotikisa wakati wa uongozi wake ni pamoja na janga la UVIKO-19 ambalo Tanzania ilipambana nalo kiustadi katika nyanja ya uchumi kupitia ushauri wa BoT.

**SWALI: Unaitazama vipi historia ya mafanikio ya Benki Kuu ya Tanzania tangu kuanzishwa kwake?**

**JIBU:** Ni muhimu kuelewa kuwa mafanikio ya Benki Kuu si jambo la usiku mmoja wala mafanikio ya gavana mmoja pekee. Ni mchakato wa kujenga hatua kwa hatua ambapo kila gavana anasimama juu ya mafanikio ya mtangulizi wake. Gavana wa kwanza marehemu Edwin Mtei aliisimamia BoT wakati wa kuanzishwa kwake na kuanzishwa kwa Shilingi ya Tanzania kuchukua nafasi ya sarafu ya Afrika Mashariki. Aliweka misingi ya taasisi ya benki kuu na usimamizi wa sera za fedha katika kipindi cha mwanzo baada ya uhuru.

Baadaye marehemu Charles Nyirabu aliiongoza Benki kwa miaka 15 katika kipindi kigumu cha mfumo wa ujamaa baada ya Azimio la Arusha la mwaka 1967 na mpito kuelekea uchumi wa soko. Naye marehemu Gilman Rutihinda alisimamia changamoto za mpito kwenda uchumi huria na mageuzi ya sekta ya fedha.

Kwa upande wa marehemu Idris Rashid, alichangia kuimarisha mifumo ya usimamizi wa taasisi za fedha wakati Tanzania ikiondoka katika udhibiti wa moja kwa moja wa uchumi. Marehemu Daudi Ballali aliendeleza mageuzi ya soko na upanuzi wa sekta ya fedha, ingawa kuondoka kwake baada ya sakata la EPA kulitikisa imani ya umma.

Ningependa pia kumzungumzia marehemu Benno Ndulu ambaye naamini alikuwa mmoja wa magavana wenye mchango mkubwa zaidi. Alirejesha imani ya umma kwa Benki Kuu, akaimarisha uthabiti wa uchumi, kupunguza mfumuko wa bei na kuchochea ujumuishaji wa kifedha kwa kuruhusu benki nyingi zaidi, huduma za uwakala wa benki na matumizi ya fedha za simu.

**SWALI: Katika kipindi chako cha uongozi, ni mafanikio gani makubwa unayoyakumbuka?**

**JIBU:** Mafanikio makubwa yalikuwa ni kuendelea kutekeleza wajibu wa kisheria wa Benki Kuu kwa mafanikio. Tulihakikisha sera za fedha zinaendelea kudhibiti mfumuko wa bei na kuleta utulivu wa uchumi. Katika kipindi changu, mfumuko wa bei uliendelea kuwa wa chini na uchumi uliendelea kukua kwa wastani mzuri.

Tulihakikisha pia uthabiti wa sekta ya fedha na usimamizi madhubuti wa benki na taasisi zisizo za benki. Kanuni za usimamizi zilisaidia kudhibiti mikopo chechefu, kuimarisha mtaji wa benki na kuongeza ujumuishaji wa kifedha. Aidha, tuliimarisha mifumo ya malipo ya kidijitali kupitia mfumo wa TIPS pamoja na kusimamia uthabiti wa thamani ya shilingi dhidi ya sarafu za kigeni.

**SWALI: Ni changamoto zipi zilikuwa kubwa zaidi katika kipindi hicho?**

**JIBU:** Changamoto ya kwanza ilikuwa matumizi makubwa ya dola nchini na kuibuka kwa soko haramu la fedha za kigeni pamoja na matumizi mabaya ya maduka ya kubadilishia fedha (bureau de change). Tulichukua hatua kali kudhibiti hali hiyo na kufanikiwa kwa kiwango kikubwa.

Pili, tulikuta maadili ya usimamizi wa benki yameporomoka na kusababisha ukiukwaji mkubwa wa taratibu. Tulifanya mageuzi makubwa ndani ya idara ya usimamizi wa benki ili kurejesha nidhamu.

Changamoto nyingine ilikuwa kuimarisha mifumo ya ndani ya Benki Kuu na uwajibikaji wa viongozi. Tulibadili mifumo ya maamuzi, tukaweka viwango vya utendaji na kuimarisha usimamizi wa ndani. Pia uhamisho wa makao makuu ya Serikali kwenda Dodoma ulihitaji Benki kufanya maboresho ya kiutawala ili kuendana na mazingira mapya.

Kulikuwa pia na changamoto za ongezeko kubwa la uchakataji wa fedha taslimu, mlipuko wa UVIKO-19, vita ya Urusi na Ukraine pamoja na kasi ya maendeleo ya teknolojia ya kifedha.

**SWALI: Benki Kuu ilisimamiaje athari za UVIKO-19?**

**JIBU:** Benki Kuu ilikuwa na jukumu la kuishauri Serikali namna ya kukabiliana na janga hilo bila kusimamisha uchumi. Tuliona kuwa kufunga kabisa shughuli za uchumi kungeleta madhara makubwa zaidi, hivyo tulishauri uchumi uendelee huku hatua za kinga zikizingatiwa.

Tulisisitiza sekta muhimu kama kilimo, usafirishaji, utalii na viwanda ziendelee kufanya kazi chini ya masharti maalumu ya afya. Pia tuliona si sahihi kupunguza kodi kwa kiwango kikubwa kwa sababu Serikali ilihitaji rasilimali nyingi zaidi kukabiliana na janga hilo.

Benki zilihimizwa kuendelea kuwa na ukwasi wa kutosha ili baada ya janga biashara ziweze kufufuka. Benki Kuu pia iliendelea kuingiza fedha za kigeni sokoni kusaidia uagizaji wa bidhaa muhimu huku ikidhibiti mianya ya matumizi mabaya ya fedha hizo.

**SWALI: Ni funzo gani kubwa lililotokana na kipindi hicho?**

**JIBU:** Tuliona kuwa hata katika changamoto kuna fursa. Tanzania iliweza kuendelea kuhudumia nchi jirani kupitia bandari zake wakati baadhi ya nchi zilifunga shughuli nyingi. Pia tulijifunza umuhimu wa teknolojia katika kuendeleza uzalishaji na huduma hata wakati wa majanga.

# ZIFAHAMU KURUGENZI ZA BENKI KUU, MAJUKUMU YAKE

Wakati Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ikiadhimisha miaka 60, zifahamu kurugenzi za taasisi hiyo zinavyobeba jukumu kubwa katika kuimarisha uchumi wa taifa, uthabiti wa sekta ya fedha na ustawi wa wananchi.

Kwa miaka yote hiyo, Benki Kuu imekuwa mhimili mkuu wa usimamizi wa fedha nchini kupitia kurugenzi zake zinazoshughulikia mifumo ya malipo, usimamizi wa sekta ya fedha, tafiti za uchumi, huduma za kibenki, usimamizi wa sarafu pamoja na huduma jumuishi za kifedha.

Taasisi hiyo iliyoanzishwa Juni 14, 1966 imegawanyika katika kurugenzi hizo ili kutekeleza kwa usahihi na vyema majukumu yake ambayo yote yana lenga kusimamia uthabiti wa uchumi. Zifuatazo ni kurugenzi zake na majukumu ya msingi;

**Kurugenzi ya Huduma za Kibenki**
Kurugenzi hii ina jukumu la kutunza akaunti na amana za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, taasisi za umma pamoja na benki za biashara.

Pia ndiyo inayosimamia mifumo mikubwa ya malipo nchini ikiwemo Tanzania Interbank Settlement System (TISS), Tanzania Automated Clearing House (TACH) na Tanzania Instant Payment System (TIPS).

Mkurugenzi wa Kurugenzi hiyo, Bw. Agathon Kipandula anasema jukumu hilo limekuwa msingi wa usalama wa fedha za umma kwa miaka mingi.

"Kwa zaidi ya miaka 15 tangu mwaka 2010 hatujawahi kupata changamoto ya upotevu wa fedha za Serikali na taasisi za umma. Hii inaonesha uimara wa mifumo yetu ya kifedha," anasema.

Aidha, anasema Benki Kuu imefanikiwa kufanya malipo yote ya Serikali bila tozo, jambo ambalo limeisaidia Serikali kuokoa fedha nyingi za matumizi ya kawaida.

"Malipo yote ya Serikali zote mbili, JMT na SMZ yanafanyika hapa Benki Kuu bila tozo yoyote. Miamala yote ya Malipo hapa Benki Kuu haitozwi tozo yoyote hivyo kuokoa fedha nyingi ya Serikali hivyo kuzipeleka kwenye sekta nyingine za umma na uzalishaji,"anasema Bw. Kipandula

Anaongeza kuwa Kurugenzi ya Huduma za Kibenki imekuwa ikitoa semina mbalimbali kwenye taasisi za umma na jamii kwa ujumla juu ya majukumu ya Benki Kuu na matumizi bora ya mifumo ya malipo ili kupunguza matumizi ya fedha taslimu.

**Kurugenzi ya Usimamizi wa Sarafu**
Kurugenzi hii ndiyo yenye jukumu la kusimamia uchapishaji, uhifadhi na usambazaji wa noti na sarafu zinazotumika nchini.

Majukumu yake pia yanajumuisha kuondoa kwenye mzunguko fedha zilizochakaa na kuhakikisha wananchi wanatumia fedha halali zenye viwango vya usalama.

Bw. Ngulingwa Balele ambaye ni murugenzi wa kurugenzi hiyo anasema jukumu hilo ni muhimu katika kulinda uchumi wa nchi.

"Tunafanya kazi kuhakikisha wananchi wanapata fedha halali na salama huku tukidhibiti uwepo wa fedha bandia kupitia alama maalumu za kiusalama," anasema.

Pia, anaongeza kuwa miongoni mwa majukumu yao ni kufanya makadirio na manunuzi ya kiwango cha noti na sarafu kinachohitajika nchini pamoja na kuhifadhi noti na sarafu katika maghala ya utunzaji fedha.

**Kurugenzi ya Tafiti na Sera za Uchumi**
Kurugenzi hii ndiyo moyo wa maandalizi ya sera za fedha nchini. Inasimamia tafiti za kiuchumi, uchambuzi wa mwenendo wa uchumi na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu masuala ya fedha na uchumi.

Kupitia kazi zake, Benki Kuu imeendelea kudhibiti mfumuko wa bei na kusaidia ukuaji wa uchumi.

Mkurugenzi wa Kurugenzi hiyo, Dkt. Suleiman Missango anasema tafiti za kiuchumi zimekuwa nyenzo muhimu ya kufanya maamuzi ya kisera.

"Tunafanya tafiti na uchambuzi wa uchumi ili kusaidia Serikali kufanya maamuzi sahihi yanayolinda thamani ya fedha za wananchi na kukuza uchumi," anasema Dkt. Missango.

**Kurugenzi ya Ustawi na Huduma Jumuishi za Fedha**
Kurugenzi hii imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanafikiwa na huduma rasmi za kifedha.

Majukumu yake yanahusisha uratibu wa huduma jumuishi za kifedha, elimu ya fedha, kushughulikia malalamiko ya watumiaji wa huduma za kifedha pamoja na kusimamia dhamana za mikopo kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati.

Bw. Kennedy Komba ambaye ni mkurugenzi wa kurugenzi hiyo anasema hatua kubwa zimepigwa katika kuwafikia wananchi na kuwajumuisha katika uchumi.

"Mwaka 2023 Watanzania waliokuwa wakifikia huduma rasmi za fedha walikuwa asilimia 89 huku wanaotumia huduma hizo wakifikia asilimia 76. Hii ni hatua kubwa ya ujumuishaji wa kifedha," anasema.

Anaongeza kuwa mfumo wa SEMA na BOT umeongeza urahisi kwa wananchi kuwasilisha malalamiko yao kwa njia za kidijitali.

Majukumu mengine ni kushirikiana na Idara ya Mawasiliano katika kutekeleza mikakati ya kutoa elimu ya fedha kwa umma na kusimamia utoaji wa dhamana ya mikopo kwa Wafanyabiashara Wadogo na wa Kati (MSMEs) kwa niaba ya Serikali.

**Kurugenzi ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha**
Kurugenzi hii ndiyo msimamizi mkuu wa benki na taasisi za fedha nchini. Inatoa leseni, kufanya ukaguzi na kuhakikisha taasisi za fedha zinafuata sheria na kanuni.

Mkurugenzi wa Kurugenzi hiyo, Bw. Sadati Musa anasema kazi hiyo ni muhimu kwa uthabiti wa sekta ya fedha. "Sekta ya fedha iliyo imara inaongeza imani kwa wananchi na kuchochea ukuaji wa uchumi wa taifa."

Shughuli nyingine ni kusajili kampuni za ukaguzi (audit firms) zinazoruhusiwa kukagua benki na taasisi za fedha zilizopewa leseni na Benki Kuu ya Tanzania.

Bw. Musa anaongeza kuwa jukumu lingine ni kushiriki katika utungaji wa sheria za kudhibiti na kusimamia sekta ya fedha, kuchambua taarifa mbalimbali zinazo wasilishwa Benki Kuu kutoka kwenye benki na taasisi za fedha (Offsite Surveillance), kufanya ukaguzi wa benki na taasisi za fedha katika sehemu zao za kazi (Onsite Examination) na kusimamia uwekezaji (financial matters) wa mifuko ya hifadhi ya jamii (social security schemes).

**Kurugenzi ya Mifumo ya Malipo ya Taifa**
Kurugenzi hii ndiyo inayosimamia mifumo yote ya malipo nchini kwa kuhakikisha miamala inafanyika kwa usalama, haraka na uhakika.

Kupitia mifumo ya TISS, TACH na TIPS, wananchi sasa wanaweza kufanya miamala ya kifedha kwa muda mfupi na kwa gharama nafuu.

Bi. Lucy Shahidi ambaye ni mkurugenzi wa kurugenzi hiyo anasema mageuzi hayo yamekuwa kichocheo kikubwa cha uchumi wa kidijitali.

"Mfumo wa TIPS umeunganisha benki na kampuni za simu hivyo kurahisisha miamala ya papo kwa papo kwa wananchi wote," anasema Bi. Lucy

Anaongeza kuwa Benki Kuu imeendelea kupunguza gharama za miamala ya kidijitali ili kuongeza matumizi ya huduma rasmi za kifedha.

Kwa ujumla, kurugenzi hizi zimeendelea kuwa nguzo muhimu katika kuhakikisha uchumi wa Tanzania unakuwa imara, salama na unaokwenda sambamba na maendeleo ya teknolojia duniani.

# Historia ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT)

| | |
|---|---|
| **Kabla ya 1905** | Tanganyika ilitumia Rupia ya Kijerumani na 'Heller' chini ya utawala wa Ujerumani huku Zanzibar ikitumia Rupia ya India chini ya serikali ya Sultani. Kubadilishana bidhaa pia kulitumika kama njia ya kufanya biashara. |
| **1905** | Benki ya Kijerumani Deutsch-Ostafrikanische Bank ilifungua ofisi yake ya kwanza Dar es Salaam ilipewa mamlaka ya kuchapisha noti na kutengeneza sarafu kwa matumizi ya Tanganyika. Kiwanda cha muda cha kutengeneza sarafu kilianzishwa Tabora. |
| **1911** | Benki nyingine iliyoitwa Handelsbank fuer Ostafrika ilianzishwa na kufungua tawi lake Tanga. |
| **1919** | Baada ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, Tanganyika iliwekwa chini ya usimamizi wa Uingereza ambapo Desemba 1919, ilianzishwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki (EACB) kusimamia noti na sarafu katika Afrika Mashariki. |
| **1936** | Zanzibar ilijiunga rasmi na Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki (EACB). |
| **1919–1966** | EACB ilisimamia utoaji wa noti na sarafu katika Tanganyika, Kenya, Uganda na Zanzibar huku thamani ya sarafu za EACB ililindwa na Pauni ya Uingereza. |
| **1965** | Bunge la Tanzania lilipitisha Sheria ya Benki Kuu Na. 12 ya mwaka 1965 ili kuwezesha kuanzishwa kwa Benki Kuu ya Tanzania |
| **Juni 14, 1966** | Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ilianza kazi rasmi ambapo EACB ilihitimisha shughuli zake wakati Tanzania, Kenya na Uganda zikiunda benki kuu zao. |
| **1978** | Sheria mpya ya Benki Kuu ya Tanzania ilitungwa, ikichukua nafasi ya marekebisho ya sheria ya awali. |
| **1995** | Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ilifanyiwa maboresho makubwa kupitia sheria mpya ya mwaka 1995. |
| **2006** | Ilitungwa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006, ambayo ndiyo msingi wa uendeshaji wa Benki Kuu hadi sasa. |
| **2026** | Benki Kuu ya Tanzania inaadhimisha Miaka 60 tangu kuanzishwa kwake (1966–2026) huku ikijivunia mchango wake katika kudumisha uthabiti wa bei, kulinda uthabiti wa sekta ya fedha, kuboresha mfumo wa sera ya fedha na kusaidia ukuaji wa uchumi jumuishi. |



# UHIFADHI WA MAZINGIRA NI NGUZO YA UCHUMI

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, akitembelea na kukagua mabanda mbalimbali ya maonesho kuhusu shughuli za uhifadhi mazingira, wakati wa Maadhimisho ya Siku ya MazingiraDuniani yanayofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete mkoani Dodoma, tarehe 05 Juni 2026.

Uhifadhi wa mazingira umeendelea kujidhihirisha kuwa moja ya nguzo muhimu ya kujenga uchumi imara na endelevu, huku Serikali ikisisitiza matumizi bora ya rasilimali za asili ili kuongeza uzalishaji, kuvutia uwekezaji na kuboresha maisha ya wananchi.

Akizungumza katika Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani Juni 5, 2026 yaliyofanyika kitaifa katika Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete jijini Dodoma, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, alisema mazingira siyo tu msingi wa uhai wa binadamu, bali pia ni rasilimali muhimu inayochochea ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi za asili ambazo zikitunzwa na kutumika kwa uendelevu zinaweza kuongeza tija katika sekta mbalimbali za uzalishaji, zikiwemo kilimo, misitu, utalii, nishati na viwanda.

Alisema mojawapo ya maeneo yenye fursa kubwa za kiuchumi ni usimamizi wa taka kupitia dhana ya uchumi rejeshi (Circular Economy), ambapo taka zinaweza kubadilishwa kuwa malighafi za kutengeneza bidhaa zenye thamani ya kiuchumi badala ya kuonekana kama mzigo kwa jamii.

"Ni muhimu kubadili mtazamo na kuziona taka kama rasilimali inayoweza kuzalisha ajira, kuongeza kipato na kuchochea ukuaji wa viwanda kupitia uzalishaji wa mbolea, chakula cha mifugo na bidhaa nyingine mbalimbali," alisema.

Aidha, Makamu wa Rais alisema matumizi ya nishati safi ya kupikia yanaendelea kuleta matokeo chanya katika uchumi wa nchi kwa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa, kuhifadhi misitu pamoja na kuboresha afya ya wananchi. Alibainisha kuwa matumizi ya nishati safi yameongezeka kutoka asilimia 6.9 mwaka 2021 hadi asilimia 28.6 mwaka 2025, hatua inayochangia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia.

Katika kuimarisha uchumi wa kijani, Makamu wa Rais alielekeza mamlaka zinazotoa vibali vya ujenzi kuhakikisha kila kibali kinaambatana na sharti la kupanda miti isiyopungua mitano. Pia alizitaka halmashauri kuanzisha na kutunza bustani za kijani ili kuboresha mazingira ya mijini na kuongeza ustahimilivu dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi.

Vilevile, aliiagiza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania kuhakikisha upatikanaji wa miche ya miti ya kutosha, huku Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni kikipewa jukumu la kushirikiana na TAMISEMI kubainisha na kusajili maeneo yenye fursa za biashara ya kaboni, sekta inayozidi kuwa chanzo kipya cha mapato na uwekezaji duniani.
Makamu wa Rais pia alisisitiza umuhimu wa taasisi za utafiti kufanya tafiti kuhusu viumbe vamizi vinavyoathiri uzalishaji katika sekta za kilimo na mifugo, akieleza kuwa tafiti hizo zitasaidia kulinda uzalishaji na kuongeza tija katika shughuli za kiuchumi.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhandisi Hamad Masauni, alisema uzinduzi wa Programu ya Mageuzi ya Kimkakati ya Mazingira Endelevu Tanzania (2026–2030) unalenga kuifanya mazingira kuwa kichocheo cha maendeleo ya uchumi kupitia urejeshaji wa uoto wa asili, kuimarisha mifumo ya ikolojia na kuongeza huduma za kiikolojia zinazotegemewa na sekta mbalimbali za uzalishaji.

Alisema programu hiyo pia inalenga kuchangia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kwa kuhamasisha upandaji wa miti bilioni mbili kila mwaka, kuongeza matumizi ya nishati safi ya kupikia, kuimarisha usimamizi wa taka, kukuza biashara ya kaboni na kuongeza ushiriki wa wanawake na vijana katika shughuli za uchumi wa kijani.

Kwa ujumla, maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani mwaka 2026 yamebeba ujumbe kwamba ukuaji wa uchumi na uhifadhi wa mazingira ni mambo yanayokwenda sambamba. Kadiri nchi inavyowekeza katika matumizi endelevu ya rasilimali za asili, ndivyo inavyojenga msingi wa uchumi shindani, unaostahimili athari za mabadiliko ya tabianchi na wenye manufaa kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Maadhimisho hayo yalifanyika chini ya kaulimbiu isemayo, "Dira 2050: Tuwajibike Kukijanisha Tanzania," yakihusisha viongozi wa Serikali, wadau wa mazingira wa ndani na nje ya nchi, taasisi za utafiti, wanafunzi na wananchi.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, akisikiliza maelezo kutoka kwa Mwanafunzi wa Shule ya Msingi Manyinga ya Mvomero, Morogoro, Jackline Eliabi kuhusu utumiaji wa taka katika kutengeneza bidhaa mbadala, wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yaliyofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete mkoani Dodoma, tarehe 05 Juni 2026.

# WAZIRI MKUU AAGIZA HALMASHAURI KUTENGA ASILIMIA 5 KUJENGA MIUNDOMBINU YA BIASHARA




Katika kuhakikisha mazingira ya biashara yanakuwa bora ili kukuza uchumi, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Mwigulu Nchemba ameelekeza halmashauri zote nchini kutenga asilimia tano ya mapato yao ya ndani kwa ajili ya ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya biashara.

Akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika Uwanja wa Ingwe Sekondari, Jimbo la Tarime Vijijini, wilayani Tarime, mkoani Mara, Jumatano, Julai 1, 2026, Waziri Mkuu alisema hatua hiyo inalenga kuondoa changamoto za maeneo ya biashara na kuongeza fursa za uzalishaji na ajira.

"Tumeenda kuweka asilimia tano kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maeneo ya biashara. Na kwenye hiyo asilimia tano, nimewaelekeza wenzetu wa TAMISEMI kwamba kama kuna eneo vijana wanalitaka kwa ajili ya kufanyia biashara, hata kama hilo eneo lina wamiliki, tumieni asilimia tano kulinunua. Msiwapeleke vijana kufanyia biashara maeneo ya mbali ambayo hayaendani na biashara wanazozifanya."

Aidha, Waziri Mkuu alisema Serikali imepitisha utaratibu wa kuwapa wafanyabiashara wanaoanzisha biashara mpya kipindi cha mwaka mmoja kabla ya kuanza kulipa kodi, ili kuwapa nafasi ya kuimarisha biashara zao.

"Wale vijana na kina mama wanaoanzisha biashara mpya hawataanza kudaiwa kodi mara wanapoanzisha biashara. Sasa watakuwa na likizo ya mwaka mzima ili wajipange katika kuimarisha biashara zao."

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu alisema Serikali itawasilisha bungeni marekebisho ya sheria inayohusu kutaifisha mifugo kwa lengo la kuondoa adhabu ambazo zimekuwa zikiwaathiri wafugaji bila kuathiri juhudi za uhifadhi.

"Bunge lijalo la mwezi wa nane tunaenda kufuta sheria inayotaifisha mifugo ya Watanzania. Tumetathmini tukagundua kwamba sheria hiyo inawatia umaskini Watanzania. Tumegundua katika baadhi ya maeneo adhabu imekuwa kubwa kuliko kosa lililotendwa."

Pia, Waziri Mkuu alisema Serikali imeelekeza kusitishwa kwa utaratibu wa kukamata vitendea kazi vya wananchi kwa madai ya faini, akisema hatua hiyo imekuwa ikikwamisha shughuli za uzalishaji na kujiongezea kipato.

"Kama mtu anadaiwa faini, mwacheni kitendea kazi chake, aendelee kufanya kazi ili awalipe faini. Tuache utekelezaji wa sheria wa kishamba shamba."

Sambamba na hayo, Waziri Mkuu alisisitiza kuwa Serikali haitavumilia ubadhirifu na matumizi mabaya ya madaraka katika utumishi wa umma.

"Mtu akiiba, mtumishi wa umma akiiba, msimhamishe. Mfukuzeni kazi. Hatuna uhaba wa watu wa kufanya kazi.

Akihitimisha, Waziri Mkuu aliwataka wananchi kuendelea kulinda amani, umoja na usalama wa nchi, akisisitiza kuwa maendeleo ya taifa na ustawi wa wananchi unategemea kuwepo kwa mazingira ya amani, utulivu na mshikamano.

# DKT MWINYI: SERIKALI INAENDELEA KUONGEZA THAMANI ZAO LA MWANI



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema Serikali inaendelea kutekeleza mikakati na juhudi maalum za kuongeza thamani ya zao la mwani, kwa lengo la kuinua kipato na kuimarisha ustawi wa kiuchumi wa wakulima wa zao hilo.

Rais Dkt. Mwinyi aliyasema hayo leo, tarehe 01 Julai 2026, alipokutana na Mratibu Mkaazi wa Umoja wa Mataifa nchini Tanzania, Ndg. Susan Ngongi Namondo, aliyefika Ikulu Zanzibar kwa mazungumzo.

Rais Dkt. Mwinyi alisema Serikali imekipa kilimo cha mwani kipaumbele, kwa kuwa ni miongoni mwa sekta muhimu za kiuchumi zinazotoa ajira na kuwawezesha wananchi wengi kuendesha maisha yao ya kila siku, hususan wanawake ambao wanaunda zaidi ya asilimia 80 ya wakulima wa zao hilo.

Alieleza kuwa, licha ya Zanzibar kuwa kitovu kikuu cha uzalishaji wa mwani nchini na kuchangia kwa kiasi kikubwa kuifanya Tanzania kuwa mzalishaji kinara wa zao hilo barani Afrika, bado sekta hiyo inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa masoko ya uhakika na kushuka kwa bei.

Alisema hali hiyo imekuwa ikiwafanya wakulima kutonufaika ipasavyo na kazi kubwa wanayoifanya katika uzalishaji wa mwani, hivyo kuathiri juhudi zao za kuongeza kipato na kuboresha maisha yao.



Rais Dkt. Mwinyi alisema Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuondokana na utaratibu wa kuuza mwani kama malighafi, ikiwemo kuanzisha na kuimarisha viwanda vya kusindika mwani ili Zanzibar iweze kuzalisha bidhaa mbalimbali zenye thamani kubwa zaidi.

Aliongeza kuwa hatua hiyo itasaidia kuongeza thamani ya zao la mwani, kupanua masoko, kuimarisha ushindani wa bidhaa za Zanzibar katika soko la kimataifa na kuongeza manufaa yanayopatikana kwa wakulima.

Rais Dkt. Mwinyi alisema Zanzibar iko tayari kufanya kazi kwa karibu na Umoja wa Mataifa pamoja na mashirika yake katika kutekeleza programu za kuendeleza kilimo cha mwani, hususan katika maeneo ya mafunzo, teknolojia, upatikanaji wa mitaji na huduma za kifedha.

Alisema ushirikiano huo utasaidia kukifanya kilimo cha mwani kuwa na tija zaidi kwa wakulima na kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa Zanzibar. Aidha, Rais Dkt. Mwinyi ameuhakikishia Umoja wa Mataifa kuwa Serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano wa muda mrefu uliopo, huku akiushukuru Umoja huo kwa mchango na msaada mkubwa unaotolewa kupitia mashirika yake, yakiwemo UNESCO, UNDP na UNICEF.

Naye Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa nchini Tanzania, Ndg. Susan Ngongi Namondo, alisema Umoja wa Mataifa unaendelea kuchukua hatua za kuimarisha kilimo cha mwani kama sehemu muhimu ya maendeleo ya sekta ya Uchumi wa Buluu. Amesema Umoja wa Mataifa utaendelea kushirikiana na Zanzibar kupitia programu mbalimbali zinazolenga kuendeleza zao la mwani, kuongeza thamani yake na kuwawezesha wakulima kunufaika zaidi kiuchumi.



# RIBA YA BENKI KUU YAONGEZEKA KUTOKA ASILIMIA 5.75 HADI 6.25




Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania akizungumza alipotangaza riba ya Benki Kuu tarehe 3 Julai, 2026 katika ofisi za BoT jijini Dar es Salaam.

Kamati ya Sera ya Fedha ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imepandisha kiwango cha Riba ya Benki Kuu (CBR) kutoka asilimia 5.75 hadi asilimia 6.25 katika robo ya tatu ya mwaka inayoanza Julai hadi Septemba 2026.

Akizungumza katika mkutano na viongozi wa benki, taasisi za fedha na waandishi wa habari, Gavana wa BoT ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Sera ya Fedha, Bw. Emmanuel Tutuba, amesema uamuzi huu unalenga kudhibiti ongezeko la mfumuko wa bei unaotokana na kupanda kwa bei za mafuta, mbolea na gharama za usafirishaji, hali inayotokana na mgogoro unaoendelea Mashariki ya Kati.

'Kamati imeona kuwa ongezeko hili la riba ya Benki Kuu ni sahihi katika kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5, na kuendelea kuchangia ukuaji wa shughuli za uchumi.". Amesema Gavana Tutuba.

Ameongeza kuwa, bei za chakula zinatarajiwa kupungua kufuatia mavuno mazuri ya msimu wa kilimo wa mwaka 2025/26. Vilevile, thamani ya shilingi inatarajiwa kuimarika kutokana na mapato yatokanayo na mauzo nje ya nchi, ikiwemo dhahabu, mazao ya kilimo, na shughuli za utalii.

"Hali hii itasaidia kupunguza bei za chakula na bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi, na hivyo kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya lengo katika nusu ya pili ya mwaka 2026".




Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mabenki Tanzania (TBA), Bw. Theobald Sabi, katika mkutano wa kutangaza Riba ya Benki KUU uliofanyika tarehe 3 Julai, 2026 katika ofisi za BoT jijini Dar es Salaam.

Kuhusu mwenendo wa uchumi nchini, Gavana Tutuba amesema uchumi umeendelea kuimarika licha ya changamoto zilizotokana na mgogoro wa Mashariki ya Kati. Tanzania Bara unakadiriwa kukua kwa asilimia 6 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2026, ukichangiwa na sekta za kilimo, ujenzi, madini, huduma za kifedha na usafirishaji, huku uchumi wa Zanzibar ukikadiriwa kukua kwa asilimia 6.6 kutokana na kuimarika kwa sekta za utalii na ujenzi.

Aidha, alieleza kuwa mfumuko wa bei kwa Tanzania Bara uliongezeka hadi asilimia 4.2 mwezi Mei 2026 kutoka asilimia 3.2 mwezi Machi, lakini uliendelea kuwa ndani ya lengo la asilimia 3–5, ukisaidiwa na ruzuku ya mafuta iliyotolewa na Serikali mwezi Mei na Juni. Zanzibar, mfumuko wa bei uliongezeka hadi asilimia 5.5 kutoka asilimia 4.9, karibu na lengo la asilimia 5.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mabenki Tanzania (TBA), Bw. Theobald Sabi, ameipongeza Benki Kuu kwa kusimamia uchumi wa nchi ambao umeendelea kukua licha ya uwepo wa migogoro ya kisiasa ulimwenguni. Aidha, ameishukuru BoT kwa uongozi madhubuti na ushirikiano unaoutoa kwa sekta ya fedha ambayo inamchango mkubwa katika kustawisha uchumi.



# TANI 28 ZA DHAHABU ZAIWEZESHA TANZANIA KUIMARISHA AKIBA YA TAIFA



Gavana Emmanuel Tutuba, akifafanua jambo kuhusu mpango wa Tanzania wa ununuzi wa dhahabu katika mkutano wa WB na IMF uliofanyika Banjul nchini Gambia kuanzia Julai 6 hadi 8, 2026

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, amesema kuwa katika kipindi cha miezi 18 iliyopita, Benki Kuu imenunua na kuhifadhi takriban tani 28 za dhahabu, zenye thamani ya dola za Marekani bilioni 3.68, sawa na shilingi trilioni 9.76.

Alisema ununuzi huo ni sehemu ya mkakati wa Serikali wa kuimarisha akiba ya fedha za kigeni, kuongeza uthabiti wa thamani ya shilingi, kuimarisha sekta ya fedha na kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi wa Taifa.

Bw. Tutuba aliyasema hayo aliposhiriki mjadala kuhusu Mikakati ya Ununuzi wa Dhahabu ya Benki Kuu ikiwa ni sehemu ya mijadala ya Mkutano wa Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), African Caucus 2026, unaozihusisha nchi 54 za Afrika, unaofanyika Banjul nchini Gambia.

Alieleza kuwa mpango wa ununuzi wa dhahabu umeiwezesha Tanzania kuongeza akiba ya dhahabu kama sehemu ya akiba ya nchi ya fedha za kigeni, sambamba na kuimarisha urasimishaji wa sekta ya madini na kukuza ujumuishi wa kifedha kwa wauzaji wa madini, hususan wachimbaji wadogo. Kupitia mpango huo, Benki Kuu imewezesha kufunguliwa kwa zaidi ya akaunti 4,000 katika taasisi mbalimbali za fedha, ikiwemo benki.

Aidha, Gavana Tutuba alisema kuwa mwitikio wa wafanyabiashara na wachimbaji wa dhahabu umeendelea kuwa mzuri kutokana na Benki Kuu kutoa bei shindani inayozingatia bei ya soko la kimataifa.

"Tunawalipa wachimbaji na wafanyabiashara wa dhahabu kwa wakati, ndani ya saa 24 tangu kufanyika kwa mauzo, na tunawalipa kwa bei ya soko la dhahabu la London ya siku hiyo, hatua inayowavutia kuiuzia dhahabu Benki Kuu." Alisema Gavana Tutuba.

Ujumbe wa Tanzania katika mkutano huo unaongozwa na Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb), na umewashirikisha pia Waziri wa Fedha na Mipango wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Dkt. Juma Malik Akil, Balozi wa Tanzania nchini Nigeria anaye hudumia pia shughuli za kibalozi katika nchi ya Gambia, Mhe. Balozi Selestine Kakele.




Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar akijadiliana jambo na Gavana Emmanuel Tutuba katika mkutano wa WB na IMF uliofanyika Banjul nchini Gambia kuanzia Julai 6 hadi 8, 2026.




Gavana Emmanuel Tutuba (wa tatu kutoka kulia) katika mjadala kuhusu Mikakati ya Ununuzi wa Dhahabu ya Benki Kuu wakati wa mkutano wa WB na IMF uliofanyika Banjul nchini Gambia kuanzia Julai 6 hadi 8, 2026.




# MFUMO WA EMS KULETA UWAZI NA UFANISI KATIKA SOKO LA JUMLA LA FEDHA ZA KIGENI



Naibu Gavana wa BoT anayesimamia Sera za Uchumi na Fedha, Dkt. Yamungu Kayandabila, akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa mfumo wa EMS uliofanyika katika ofisi za BoT jijini Dar es Salaam.



Mkurugenzi wa Masoko ya Fedha wa BoT, Bw. Emmanuel Akaro, akizungumza katika uzinduzi wa mfumo wa EMS uliofanyika katika ofisi za BoT jijini Dar es Salaam.



Naibu Gavana wa BoT, Dkt. Yamungu Kayandabila katika picha ya pamoja na wafanyakazi wa BoT pamoja na wawakilishi kutoka kwenye Mabenki mara baada ya uzinduzi wa mfumo wa EMS.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT), tarehe 08 Juni 2026, imezindua Mfumo wa Kielektroniki wa Kuoanisha Miamala (Electronic Matching System – EMS) katika Soko la Jumla la Fedha za Kigeni (Interbank Foreign Exchange Market -(IFEM) ambao utawawezesha washiriki wa soko hilo kuwasilisha, kuoanisha na kufanya miamala ya fedha za kigeni kwa njia ya kielektroniki.

Washiriki wa mfumo huu ni mabenki ya biashara na wauzaji wakubwa wa bidhaa nje ya nchi (large exporters) watakaoidhinishwa na BoT kushiriki katika soko kupitia mfumo huu.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo Naibu Gavana wa BoT anayesimamia Sera za Uchumi na Fedha, Dkt. Yamungu Kayandabila, alisema mfumo huo unaoendeshwa kwa kuzingatia kanuni na taratibu zilizowekwa na kusimamiwa na BoT utaongeza uwazi na ufanisi katika upatikanaji wa viwango vya kubadilisha fedha za kigeni.

“Kupitia mfumo huu, tunatarajia kuongezeka kwa uwazi wa soko na kuchochea ufanisi katikaupatikanaji wa viwango vya kubadilisha fedha. Aidha, tunategemea kuongezeka kwa ukwasi, kuimarisha ushindani, na kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa soko”.

Aliongeza kuwa mfumo wa EMS utaimarisha uwezo wa Benki Kuu katika ufuatiliaji wa shughuli za soko na kusaidia kuhakikisha kuwa soko la fedha za kigeni linaendelea kufanya kazi kwa utulivu, ufanisi na kwa kuzingatia viwango bora vya kimataifa.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Masoko ya Fedha, Bw. Emmanuel Akaro alieleza kuwa kupitia mfumo huu, washiriki watafanya biashara ya fedha za kigeni kwa mfumo wa kutotambulika (anonymous trading), ambapo oda za ununuzi na uuzaji zitaoanishwa moja kwa moja kwa kuzingatia kigezo cha bei na muda wa kuwasilishwa kwa oda husika (price-time priority)

Alisisitiza kuwa mfumo huu utatumika mahsusi kwa utekelezaji wa miamala ya fedha za kigeni ya papo kwa papo (spot transactions) kati ya Shilingi ya Tanzania (TZS) na Dola ya Marekani (USD).

Soko la fedha za kigeni hapa nchini limekuwa na mafanikio makubwa tangu kutungwa kwa Sheria ya Fedha za Kigeni ya mwaka 1992.

Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na kutungwa kwa Sera ya Ushiriki wa Benki Kuu katika Soko la Jumla la Fedha za Kigeni ya 2023 iliyolenga kuweka mfumo wa ushiriki wa Benki Kuu katika soko na kuimarisha utulivu wa shughuli za ubadilishaji wa fedha za kigeni.

Pia, Kanuni za Maadili ya Soko la Jumla la Fedha za Kigeni za mwaka 2024, zilizojumuisha kanuni 52 zinazotambuliwa kimataifa. Kanuni hizi zinalenga kuimarisha uwazi, uadilifu, weledi na uzingatiaji wa viwango bora vya kimataifa katika shughuli za soko la fedha za kigeni nchini.

# ELIMU YA FEDHA YATAJWA NGUZO MUHIMU YA UJUMUISHI WA KIFEDHA

Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), anayesimamia Uthabiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Bi. Sauda Msemo, amesisitiza umuhimu wa kuendelea kuimarisha elimu ya fedha nchini ili kuwawezesha wananchi kutumia kwa ufanisi huduma mbalimbali za kifedha na hivyo kuongeza kiwango cha ujumuishi wa kifedha.

Akifungua Jukwaa la Elimu ya Fedha lililofanyika tarehe 29 Juni 2026 katika ofisi za BoT jijini Dar es salaam, Naibu Gavana alisema jukwaa hilo linatoa fursa muhimu ya kutathmini hatua zilizofikiwa katika kuifanya elimu ya fedha kuwa sehemu ya utaratibu endelevu kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Alieleza kuwa matokeo ya utafiti wa FinScope 2023 yanaonesha kuwa kiwango cha ujumuishi wa kifedha nchini kimefikia asilimia 76, mafanikio yaliyotokana kwa kiasi kikubwa na ukuaji wa huduma za fedha kwa simu.

Utafiti pia ulionesha kuwa uelewa wa fursa mbalimbali za huduma za kifedha na uwekezaji ulikuwa chini.

"Hata hivyo, juhudi zinazoendelea za kutoa elimu ya fedha ikiambatana na uhamasishaji wa fursa zilizopo zinaleta matunda, ambapo uelewa unakua kwa kasi kubwa". Alieleza Naibu Gavana huyo.

Alisisitiza  kuwa utekelezaji wa programu ya Wakufunzi wa Elimu ya Fedha umeendelea kuleta mafanikio makubwa, ambapo hadi sasa jumla ya wakufunzi 1,736 wameidhinishwa kutoa elimu hiyo katika maeneo mbalimbali nchini.

"mafanikio hayo yametokana na ushirikiano madhubuti kati ya BoT na taasisi 14 za elimu zinazotekeleza programu ya mafunzo ya Wakufunzi wa Elimu ya Fedha, nazipongeza kwa mchango wao katika kuwajengea uwezo wataalamu watakaosaidia kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu masuala ya fedha".

Aidha, alisema jitihada hizo zinaendana na Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa mwaka 2020/21–2029/30 ulioandaliwa na Wizara ya Fedha, ambao unaweka msisitizo katika kuimarisha elimu na uelewa wa masuala ya fedha nchini.

Aliongeza kuwa kupitia Baraza la Taifa la Ujumuishi wa Huduma za Kifedha, wadau mbalimbali wameendelea kushirikiana kutekeleza Mkakati wa Tatu wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha (NFIF III), ambapo elimu ya fedha imepewa nafasi ya kimkakati katika kuongeza matumizi ya huduma rasmi za kifedha.

Jukwaa hilo lenye kauli mbiu 'Elimu ya fedha kwa maendeleo Yetu Sote'  limewakutanisha wadau na washirika kutoka sekta ya fedha, taasisi za elimu, Serikali na washirika mbalimbali kwa lengo la kutathmini mafanikio yaliyopatikana, kubadilishana uzoefu na kuweka mikakati ya kuendelea kuimarisha utoaji wa elimu ya fedha nchini.



Naibu Gavana wa BoT, Bi. Sauda Msemo, akizungumza katika Jukwaa la Elimu ya Fedha lililofanyika tarehe 29 Juni 2026 katika ofisi za BoT jijini Dar es Salaam.




Naibu Gavana wa BoT, Bi. Sauda Msemo, akizungumza katika Jukwaa la Elimu ya Fedha lililofanyika tarehe 29 Juni 2026 katika ofisi za BoT jijini Dar es Salaam.



# IMF YATOA TATHMINI CHANYA, TANZANIA KUNUFAIKA NA DOLA MILIONI 375.5



Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), na Serikali ya Tanzania zimefikia makubaliano ya ngazi ya wataalamu kuhusu kukamilika kwa tathmini za mwisho za programu za Mfuko wa Mikopo Nafuu (ECF) na Mfuko wa Ustahimilivu na Uendelevu (RSF). Hatua hii itawezesha Tanzania kupata ufadhili wa takribani dola za Marekani milioni 375.5 baada ya kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya IMF.

Fedha hizo zitachangia jumla ya msaada wa dola bilioni 1.052 kupitia ECF kwa ajili ya kuimarisha uchumi na sekta za uzalishaji na huduma za jamii, pamoja na dola milioni 563.8 kupitia RSF kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi tangu kuanza kwa programu hizo.

Taarifa hiyo imetolewa na IMF kupitia Kiongozi wa Timu yake ya Wataalamu, Nicolas Blancher, kufuatia kikao cha kuhitimisha ziara ya timu hiyo kilichofanyika tarehe 12 Mei 2026 katika Benki Kuu jijini Dar es Salaam. Katika kikao hicho, upande wa Tanzania uliongozwa na Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb), na pia kilihudhuriwa na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba.

Bw. Blancher alisema IMF imeridhishwa na utekelezaji wa programu hizo, akibainisha kuwa malengo makuu ya kiuchumi yamefikiwa kwa kiwango kikubwa. Alieleza kuwa uchumi umeendelea kukua kwa kasi, mfumuko wa bei umebaki ndani ya lengo la Benki Kuu ya Tanzania, na akiba ya fedha za kigeni iko katika kiwango cha kuridhisha.

Aidha, alibainisha kuwa matumizi ya Serikali katika sekta za elimu na afya yameongezeka, sambamba na hatua za kuimarisha ustahimilivu dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi. Uchumi wa Tanzania unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.9 mwaka 2026 huku mfumuko wa bei ukibaki kati ya asilimia 3 hadi 5.

Kwa mtazamo wa muda wa kati na mrefu, IMF imeeleza kuwa Tanzania ina nafasi nzuri ya kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo 2050 iwapo itaendeleza mageuzi ya kukuza rasilimali watu, kuboresha mazingira ya biashara, kuimarisha usimamizi wa fedha za umma na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi.

Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar, alihakikisha kuwa Serikali itaendelea kutekeleza programu hizo kwa umakini ili kuhakikisha uchumi unaendelea kuwa imara, jumuishi na wenye tija kwa maendeleo ya taifa.



Gavana Emmanuel Tutuba akizungumza jambo na Mwakilishi Mkazi wa IMF, Bw. Sebastian Acevedo, katika kikao cha kuhitimisha ziara ya Timu hiyo kilichofanyika tarehe 12 Mei 2026 BoT jijini Dar es Salaam.



Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb) akizungumza katika kikao na Timu ya Wataalamu kutoka IMF kilichofanyika tarehe 12 Mei 2026 BoT jijini Dar es Salaam.

# BODI YA WAKURUGENZI BoT YAKUTANA NA WAZIRI WA FEDHA



Gavana Emmanuel Tutuba akifafanua jambo kwa Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb) katika kikao na Bodi ya Wakurugenzi ya BoT kilichofanyika katika ofisi za Wizara ya Fedha jijini Dodoma, tarehe 18 Juni 2026.

Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ikiongozwa na Mwenyekiti wake ambaye pia ni Gavana wa Benki Kuu, Bw. Emmanuel Tutuba, ilimtembelea Waziri wa Fedha Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar katika ofisini kwake jijini Dodoma.

Ziara hiyo ya bodi yenye lengo la kufanya nae mazungumzo kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu utekelezaji wa majukumu ya BoT ilifanyika Juni 18, 2026 jijini Dodoma.

Akizungumza katika kikao hicho, Mhe. Balozi Omar alisisitiza kuwa Benki Kuu ina nafasi muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, kwa kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji, ukuaji wa sekta binafsi, pamoja na maendeleo jumuishi ya uchumi.

Aidha, aliipongeza Benki Kuu kwa usimamizi thabiti wa sekta ya fedha, hususan benki za biashara, hatua iliyochangia kupungua kwa kiwango cha mikopo chechefu hadi kufikia chini ya asilimia 5. Pamoja na pongezi hizo, alihimiza Benki Kuu kuendelea kufanya maboresho na mageuzi zaidi katika sekta ya fedha ili kuongeza mchango wake katika kukuza uchumi wa Taifa.

Kwa upande wake, Gavana Tutuba alieleza kuwa Benki Kuu itaendelea kutekeleza kwa uthabiti sera ya fedha, pamoja na kudhibiti mfumuko wa bei, ili kuhakikisha uwepo wa mazingira wezeshi ya ukuaji endelevu wa uchumi wa nchi.

Katika hatua nyingine, Bodi hiyo iliendesha vikao vyake katika Makao Makuu ya Benki Kuu jijini Dodoma kuanzia tarehe 18 hadi 19 Juni 2026. Katika kipindi hicho, wajumbe wa Bodi walipata pia fursa ya kutembelea kiwanja cha Benki Kuu kilichopo katika Mji wa Serikali, Mtumba, ambapo waliongozwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Mhe. Prof. Palamagamba J.A. Kabudi.



Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb) akizungumza katika kikao na Bodi ya Wakurugenzi ya BoT kilichofanyika katika ofisi za Wizara ya Fedha jijini Dodoma, tarehe 18 Juni 2026.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Mhe. Prof. Palamagamba J.A. Kabudi akizungumza jambo na Gavana Emmanuel Tutuba, walipotembelea kiwanja cha BoT katika Mji wa Serikali, Mtumba tarehe 19 Juni 2026.



Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb) akizungumza katika kikao na Bodi ya Wakurugenzi ya BoT kilichofanyika katika ofisi za Wizara ya Fedha jijini Dodoma, tarehe 18 Juni 2026.

# BOT YARATIBU MKUTANO WA KIDUNIA UJUMUISHAJI WA KIFEDHA




Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bi. Sauda Msemo, akizungumza katika mkutano wa AFI uliofanyika jijini Arusha kuanzia tarehe 11 hadi 14 Mei 2026.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeratibu mkutano wa kimataifa wa nchi wanachama wa Muungano wa Ujumuishaji wa Kifedha (AFI), uliofanyika jijini Arusha, ukiwa na lengo la kuboresha sera za fedha ili ziwe jumuishi zaidi.

Mkutano huo ulifunguliwa rasmi tarehe 11 Mei 2026 na Naibu Gavana wa BoT anayeshughulikia Uthabiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Bi. Sauda Msemo, ambaye alisisitiza kuwa mkutano huo utakuwa suluhisho la changamoto ya upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kupitia mijadala itakayofanyika.

Mkutano huo, ulitamatika Alhamisi, tarehe 14 Mei 2026, uligawanyika katika vikundi kazi viwili: kimoja kikijikita katika Viwango vya Kimataifa vya Uwiano katika Sera (GSP), na kingine kikijadili Ufadhili kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati (SMEF).

Akizungumza katika ufunguzi huo, Bi. Msemo alisema kuwa mkutano huo unalenga kuangalia namna bora ya kusaidia wanawake na makundi maalum ya wajasiriamali kupitia sera jumuishi na kanuni rafiki.

Alibainisha kuwa katika nchi nyingi, wanawake wanakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo ukosefu wa dhamana, haki za ardhi, pamoja na changamoto za ujumuishwaji wa kidijitali.

Licha ya changamoto hizo, Bi. Msemo alieleza kuwa Tanzania imepata mafanikio makubwa katika safari ya ujumuishi wa kifedha.

"Kupitia Mfumo wa Taifa wa Ujumuishi wa Kifedha wa mwaka 2023–2028, malengo madhubuti yamewekwa na yanaendelea kutekelezwa katika maeneo ya upatikanaji, matumizi, ubora wa huduma na ustawi wa kifedha," alifafamua.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Sera, Programu na Utekelezaji wa AFI, Dkt. Eliki Boletawa, alisema kuwa ushirikiano kati ya nchi wanachama ni muhimu katika kuhakikisha kuwa sera za kifedha zinakuwa jumuishi zaidi na zinawafikia wananchi wengi zaidi.

Ikumbukwe kuwa, katika kuonesha mafanikio ya ujumuishi wa kifedha, mwaka 2025 BoT ilipokea tuzo ya ubunifu katika ujumuishi wa kifedha, inayojulikana kama Nestor Espenilla Jr. Award.



Washiriki wa Mkutano wa AFI wakifuatilia mkutano huo uliofanyika tarehe 11 hadi 14 Mei 2026 jijini Arusha.




Naibu Gavana wa BoT, Dkt. Rahma Mahfoudh (kulia) katika kikao cha Bodi ya Chuo cha Benki Kuu, kushoto ni mkuu wa chuo hicho, Dkt. Nicas Yabu.

# DKT. MAHFOUDH AONGOZA KIKAO BODI YA CHUO CHA BENKI KUU

Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) anayeshughulikia Utawala na Udhibiti wa Ndani, Dkt. Rahma Mahfoudh, ameongoza kikao cha kawaida cha Bodi ya Chuo cha Benki Kuu kwa mara ya kwanza tangu kuteuliwa kwake kushika wadhifa huo Januari 29, 2026.

Kikao hicho kilichofanyika Alhamisi, Aprili 30, 2026, kilihudhuriwa na wajumbe wa bodi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar, ambapo walijadili masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo na uendeshaji wa chuo hicho.

Awali, Mkuu wa Chuo cha Benki, Dkt. Nicas Yabu, alimkaribisha Naibu Gavana na kumtembeza katika maeneo ya chuo hicho, sambamba na kumtambulisha kwa wafanyakazi, menejimenti na wanafunzi.

Katika ziara hiyo, Dkt. Mahfoudh alikagua miundombinu mbalimbali ya chuo, ikiwemo ujenzi wa jengo la huduma jumuishi (multipurpose building), ambapo alisisitiza umuhimu wa kusimamia kwa karibu utekelezaji wa mradi huo ili ukamilike kwa wakati uliopangwa.

"Mkuu wa Chuo, simamieni mradi huu ujengwe kwa ufanisi na ukamilike kwa wakati ili Benki ianze kunufaika na jengo hili kama ilivyopangwa hapo awali," alisema Dkt. Mahfoudh.

Wakati huo huo, Chuo cha Benki Kuu kuanzia Aprili 27 hadi 29, 2026 kilipokea ugeni kutoka Benki Kuu ya Malawi (RBM) uliolenga kujifunza kuhusu uendeshaji wa chuo hicho.

Ujumbe huo uliongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa RBM, Bi. Tiyamike Kaphuka, ambaye alikishukuru chuo kwa kuwapa fursa ya kujifunza na kubainisha kuwa watafanyia kazi maarifa waliyoyapata.

Alisema uzoefu walioupata utakuwa chachu katika maandalizi ya kuanzisha chuo cha Benki Kuu ya Malawi, hatua inayolenga kuimarisha uwezo wa rasilimali watu katika sekta ya fedha nchini humo.



Naibu Gavana wa BoT, akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Bodi ya Chuo cha Benki Kuu katika kikao kilichofanyika Aprili 30 2026.



# TANZANIA KUIMARISHA SAFARI YA UCHUMI USIO TEGEMEA FEDHA TASLIMU




Kikao cha 13 cha Jukwaa la Uthabiti wa Sekta ya Fedha kilichofanyika tarehe 28 Aprili 2026 chini ya uongozi wa Mwenyekiti wa Jukwaa hilo ambaye pia ni Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, kimejadili masuala muhimu katika sekta ya fedha na kukubaliana kuharakisha mchakato wa kuijenga Tanzania kuelekea uchumi unaotumia fedha taslimu kwa kiwango kidogo zaidi.

Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa ni Mfumo wa Usimamizi wa Majanga wa Sekta ya Fedha, Mfumo wa Usalama wa Kidijitali katika Sekta ya Fedha, pamoja na Ripoti ya Uthabiti wa Sekta ya Fedha 2025.

Katika eneo la mfumo wa usimamizi wa majanga katika sekta ya fedha, jukwaa lilijadili namna bora ya kuimarisha uratibu katika maandalizi, usimamizi na utatuzi wa migogoro, kwa kuzingatia mbinu bora za kimataifa ikiwemo miongozo ya Bodi ya Uthabiti wa Kifedha.

Aidha, jukwaa lilijadili uwezekano wa kuanzishwa kwa mfuko wa ulinzi wa wamiliki wa bima, mfuko wa ulinzi wa wawekezaji, pamoja na mipango ya dhamana ya akiba kwa vyama vya ushirika wa akiba na mikopo (SACCOs), ili kusaidia utatuzi kwa gharama ndogo na kuimarisha imani katika sekta ya fedha.

Katika eneo la usalama wa kidijitali, Jukwaa lilipokea na kujadili kuhusu Vithibiti vya kiufundi na kiutendaji vya usalama wa mtandao ikiwemo mifumo ya kinga dhidi ya mashambulizi ya mtandao, usimamizi wa vihatarishi vya kidijitali, ufuatiliaji wa miamala na mifumo, pamoja na hatua za kuimarisha mwendelezo wa huduma za kifedha wakati wa matukio ya dharura.

Jukwaa lilikubaliana kuwa uimarishaji wa hatua hizo ni muhimu katika kulinda uthabiti wa sekta ya fedha sambamba na kuendeleza matumizi salama ya huduma za kifedha za kidijitali, hususan katika safari ya kuelekea uchumi wa matumizi kidogo ya fedha taslimu.

Aidha, Jukwaa lilipendekeza kubuniwa kwa mkakati mahsusi utakaoharakisha kufikiwa kwa lengo hilo nchini, hatua inayotarajiwa kuongeza ufanisi wa mifumo ya malipo, kupunguza gharama za miamala, kuimarisha ujumuishaji wa kifedha na kuchochea ukuaji wa uchumi wa kidijitali.

Jukwaa hilo linawakutanisha wajumbe 15 kutoka ofisi mbalimbali za serikali pamoja na taasisi zinazosimamia sekta ya fedha, likiwa na lengo la kuimarisha uratibu na ushirikiano katika kulinda uthabiti wa sekta ya fedha nchini.

# BOT YAWANOA WAJUMBE KAMATI YA BAJETI KUHUSU DHAMANA ZA



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mhe. Mashimba Ndaki akitoa maelekezo katika wasilisho la BoT.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imewasilisha mada kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu dhamana za Serikali, ikieleza umuhimu wake katika kugharamia miradi ya maendeleo na mchango wake katika kuimarisha uchumi wa nchi.

Akiwasilisha mada hiyo Alhamisi Juni 25, 2026, Mkurugenzi wa Masoko ya Fedha wa BoT, Bw. Emmanuel Akaro, alisema dhamana za Serikali zimekuwa nyenzo muhimu ya kuipatia Serikali rasilimali fedha zinazowezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema BoT inaendelea kuboresha mfumo wa uwekezaji katika dhamana za Serikali ili kupanua wigo wa washiriki na kuongeza fursa za uwekezaji.

"Kwa sasa tunaandaa maboresho ya kanuni yatakayoruhusu ushiriki wa wawekezaji kutoka sehemu mbalimbali duniani. Hivi sasa, washiriki wanaoruhusiwa ni Watanzania, raia wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)," alisema Bw. Akaro.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Mashimba Ndaki, aliipongeza Benki Kuu ya Tanzania kwa mchango wake katika kusimamia uthabiti wa uchumi wa nchi na maendeleo ya sekta ya fedha.

BoT inaendelea kushirikiana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kupitia vikao vya kujengeana uwezo vinavyolenga kuwawezesha wabunge kufahamu kwa kina masuala mbalimbali ya sekta ya fedha, hatua inayochangia kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa sera za uchumi nchini.



Mkurugenzi wa Masoko ya Fedha BoT, Bw. Emmanuel Akaro akitoa wasilisho mbele ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Bajeti.




Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Laurent Luswetula akizungumza katika wasilisho la BoT mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti.



# GAVANA TUTUBA: UTHABITI WA UCHUMI NI MATOKEO YA USIMAMIZI THABITI WA BOT




Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba, amesema uthabiti wa uchumi wa Tanzania, unaodhihirishwa na mfumuko wa bei unaobaki katika kiwango cha takriban asilimia 4, ni matokeo ya usimamizi madhubuti wa sera za fedha na mifumo ya kifedha inayotekelezwa na Benki Kuu.

Akizungumza baada ya kutembelea banda la BoT katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa (Saba Saba) yanayoendelea katika Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, tarehe 10 Julai 2026, Gavana Tutuba alisema maonesho hayo yanatoa fursa kwa wananchi kujifunza kuhusu kazi za Benki Kuu na mchango wake katika maendeleo ya uchumi wa nchi.

Gavana Tutuba amebainisha kuwa uamuzi wa hivi karibuni wa kuweka kiwango cha riba ya Benki Kuu kuwa 6.25% unalenga kuhakikisha kunakuwa na ukwasi wa kutosha katika sekta ya benki, kukuza utoaji wa mikopo na kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5.

Alisema Tanzania imeendelea kuwa na uchumi imara unaovutia wawekezaji licha ya changamoto za kiuchumi duniani, huku akieleza kuwa mafanikio hayo yanatokana na usimamizi wa kitaalamu wa sera za fedha, mifumo salama ya malipo na uwekezaji endelevu katika kuwajengea uwezo wataalamu wa Benki Kuu.

Katika ziara hiyo, alipata pia maelezo kuhusu mfumo wa Sema na BoT, ambao umeongeza ufanisi katika upokeaji na utatuzi wa malalamiko ya watumiaji wa huduma za kifedha. Aliagiza mfumo huo uendelee kuboreshwa ili uweze kuwafikia wananchi wengi zaidi, wakiwemo wasioweza kutumia mifumo ya kidijitali kwa urahisi.

Gavana Tutuba alisema Benki Kuu inajivunia mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 60 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1966, ikiwemo kuimarika kwa uthabiti wa sekta ya fedha, kuongezeka kwa ujumuishaji wa kifedha, kuimarika kwa mifumo ya malipo na kuongezeka kwa taasisi za fedha zinazotoa huduma kwa wananchi nchini.





# BOT YAIBUKA KINARA SABA SABA KATIKA KUNDI LA TAASISI ZA USIMAMIZI






Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dennis Londo, akikabidhi tuzo ya BoT kwa Meneja Msaidizi, Idara ya Mawasiliano BoT, Bi. Noves Moses, katika hafla ya kufunga maonesho ya Saba Saba iliyofanyika tarehe 13 Julai 2026.




Washiriki wa BoT katika maonesho ya Saba Saba waliowezesha Benki Kuu kupata tuzo ya banda bora katika kundi la Taasii za Usimamizi wakiongozwa na Meneja Mawasiliano BoT, Bi. Victoria Msina.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeibuka mshindi wa kwanza wa banda bora katika kundi la Taasisi za Usimamizi kwenye Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa (Saba Saba), yaliyofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Julius K. Nyerere, Barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 28 Juni hadi 13 Julai 2026.

Tuzo hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dennis Londo, katika hafla ya kufunga maonesho hayo iliyofanyika tarehe 13 Julai 2026. Kwa niaba ya Benki Kuu ya Tanzania, tuzo hiyo ilipokelewa na Meneja Msaidizi, Idara ya Mawasiliano BoT, Bi. Noves Moses.

Ushindi huo unatokana na ubora wa maandalizi ya banda la Benki Kuu pamoja na huduma za elimu kwa umma zilizotolewa kwa wageni waliotembelea banda hilo katika kipindi chote cha maonesho.

Kupitia banda lake, Benki Kuu ilitoa elimu kwa umma kuhusu majukumu yake ya msingi katika kusimamia ukuaji endelevu wa uchumi wa Taifa, ikiwemo utekelezaji wa sera ya fedha, kudumisha uthabiti wa bei, kusimamia sekta ya fedha na mifumo ya malipo, pamoja na kuhamasisha ujumuishi wa kifedha kwa maendeleo ya wananchi na uchumi kwa ujumla.

Katika kipindi chote cha maonesho, banda la Benki Kuu ya Tanzania lilitembelewa na zaidi ya wananchi 15,000, wakiwemo viongozi mbalimbali wa Serikali, wawakilishi wa taasisi za umma na binafsi, mabalozi, wanafunzi na wadau wengine. Wageni hao waliopata fursa ya kupata elimu, kuuliza maswali na kupatiwa ufafanuzi kuhusu shughuli na huduma zinazotolewa na BoT.

Tuzo hiyo ni uthibitisho wa ubunifu, weledi na kujituma kwa watumishi wa Benki Kuu ya Tanzania walioshiriki katika maandalizi na uendeshaji wa banda hilo. Aidha, inaakisi dhamira ya Benki Kuu ya kuendelea kutoa huduma bora kwa umma, kuimarisha mawasiliano na wadau wake, na kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi, kwa wakati na kwa uwazi kuhusu sera, majukumu na huduma mbalimbali zinazotolewa na Benki Kuu.

# VIBONZO


Mke Wangu upo wapi?, Nimetoka kupokea simu ya mtu anasauti kama wewe, anasema amepata ajali nimtumie laki 3.
UTAWALA
Ajali? Mimi nipo nyumbani sasa hivi. Hao watakuwa ni matapeli, mume wangu. Wanatumia Akili Unde (AI) kuiga sauti za watu. Wanachukua sauti hizo kutoka kwenye mitandao ya kijamii au kwa kupiga simu kwa namba ngeni, kisha wanazitumia kuwatapeli watu.
60TH ANNIVERSARY 1966 - 2026


Bw. Mabushi, leo muda wa zawadi nataka nimwage noti mpaka steji yote ifunikwe! Watu wajue mimi ni Tajiri wa kweli!
Wewe Masalu! Utajiri wa kweli sio kumwaga fedha chini kaka, unapaswa kuithamini kama tunu ya taifa. Nakushauri uziweke kwenye chombo maalum kilichoandaliwa.
Karibu kwenye harusi ya Nyangeta masalu
10000
10000

# WANANCHI WANUFAIKA NA ELIMU INAYOTOLEWA NA BOT SABASABA









Wananchi waliotembelea Banda la Benki Kuu ya Tanzania (BoT) katika Maonesho ya 60 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) yanayoendelea katika Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, wamenufaika na elimu ya majukumu ya BoT pamoja na elimu ya masuala mbalimbali ya fedha.

Bi. Zainab Mtweve kutoka Morogoro ni miongoni mwa waliotembelea banda hilo na amesema elimu kuhusu utunzaji wa akiba, mikopo na uwekezaji katika dhamana za serikali itamsaidia katika kusimamia fedha zake kwa ufanisi na uwekezaji wa baadae.

Kwa upande wake, Bw. Ahmed Wazir Mohamed mkazi wa Bunju jijini Dar es salaam, amesema kwa kutembelea banda hilo amepata elimu ya namna Benki Kuu inadhibiti mfumuko wa bei kwa kutumia Sera ya fedha. Aidha

Pia, kuhusu majukumu mengine ya BoT amabayo ni kutoa sarafu ya nchi ambayo ni Shilingi ya Tanzania, kusimamia na kudhibiti mabenki na taasisi za fedha, kusimamia na kudhibiti mifumo ya malipo nchini,kuhifadhi akiba ya nchi ikiwemo fedha za kigeni.

Vilevile, wananchi wanaelezwa kuhusu utaratibu wa kushughulikia malalamiko ya watumiaji wa huduma za kifedha masuala ya ajira na utumishi ndani ya Benki Kuu, pamoja na fursa za masomo zinazotolewa na Chuo cha BoT.

Maonesho hayo, yenye kaulimbiu isemayo, "Maonesho ya Biashara ya Kimataifa Sabasaba, Fahari ya Tanzania," yalianza Juni 28, 2026 na yanatarajiwa kuhitimishwa Julai 13, 2026.

# GAVANA BOT AITAKA BODI YA BIMA YA AMANA KUFANYA KAZI NA MABENKI KUELIMISHA KUHUSU KINGA YA AMANA INAYOTOA KWA




Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, akipokea zawadi maalumu baada ya kutembelea banda la DIB katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam tarehe 10 Julai 2026.

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, ameitaka Bodi ya Bima ya Amana (DIB) kuongeza kasi ya elimu kwa umma kuhusu majukumu yake ikiwa ni pamoja na kushirikiana na benki kuwaelimisha wananchi.

Ametoa wito huo tarehe 10 Julai 2026 wakati alipotembelea banda la DIB katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam(Sabasaba).

"Ongezeni kasi ya utoaji wa elimu kwa umma na kubuni mbinu za mawasiliano zitakazoongeza uelewa wa wananchi kuhusu mfumo wa Bima ya Amana," aliagiza Gavana Tutuba ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa DIB.

Katika hatua ya kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu mfumo wa ulinzi wa amana zao, Gavana alishauri DIB kushirikiana na mabenki yote nchini kuweka nembo rasmi ya DIB pamoja na ujumbe mfupi unaoeleza kuwa amana zilizoko benki zinakingwa na Bodi ya Bima ya Amana.

"Ni vyema DIB ikaona uwezekano wa kushirikiana na mabenki ili mteja anapofika kufungua akaunti, au anaposoma fomu yoyote ya kibenki, aone nembo ya DIB na ujumbe unaoeleza kuwa amana zao zinalindwa na Bodi ya Bima ya Amana. Hii itaongeza uelewa wa wananchi na kuimarisha imani yao katika mfumo wa benki," alisema Gavana.

Aidha, Gavana alisisitiza kuwa, shughuli ya utoaji wa elimu ya fedha iwe endelevu na ilenge kuwafikia wananchi wa mijini na vijijini kwa kutumia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, maonesho ya biashara, vibonzo, semina na njia nyingine za mawasiliano.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuhakikisha Watanzania wengi zaidi wanaelewa manufaa ya mfumo wa Bima ya Amana ambao utapelekea kuongeza matumizi ya huduma rasmi za kifedha na kuimarisha imani ya umma katika sekta ya benki.

Gavana Tutuba alisema pamoja na ukuaji wa sekta ya fedha nchini, bado kuna haja ya kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanafahamu namna amana zao zinavyolindwa wanapoweka fedha katika benki na taasisi za kifedha.

Mapema Gavana Tutuba alipata maelezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya DIB katika uelimishaji wa umma na mchango wake katika kulinda amana za wateja wa benki na kuimarisha uthabiti wa sekta ya fedha nchini.

Maelezo hayo yalitolewa na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa Umma na Mawasiliano wa DIB, Bw. Lwaga Mwambande, ambaye alimweleza Gavana kuhusu mfumo wa Bima ya Amana pamoja na majukumu makuu ya Bodi, ikiwa ni pamoja na jukumu jipya la kupunguza hasara katika mchakato wa utatuzi wa mgogogro au mdororo katika uendeshaji inayojitokeza katika benki au taasisi za fedha.

Aidha, alimweleza Gavana kuhusu mikakati mbalimbali inayotekelezwa na DIB katika kuongeza uelewa wa umma kuhusu ulinzi wa amana, ikiwemo kuwafikia wananchi kupitia maonesho ya biashara, vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na programu mbalimbali za uelimishaji umma.

Bodi ya Bima ya Amana inashiriki katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ikiwa na banda lake lenyewe kwa mara ya pili. Mara ya kwanza ikiwa ni mwaka 2025 ambapo ilihudumia zaidi ya wananchi 12,000.

# BOT YASHIRIKI MAONESHO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA






Katika kuhakikisha jamii inafikiwa na kufahamu majukumu yake, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeshiriki Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika mkoani Dodoma katika Viwanja vya Chinangali kuanzia Juni 16 hadi Juni 23, 2026.

Maonesho hayo yaliyokuwa na kauli mbiu iliyosema 'Kuchochea uwajibikaji jumuishi kwa huduma endelevu' yalifunguliwa rasmi Jumanne Juni 17, 2026 na Waziri wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete.

Akifungua maonesho hayo, Mhe. Kikwete alisema maonesho hayo yatumike kama eneo ambalo wananchi watapata huduma kwa urahisi, weledi na uharaka katika taasisi husika za Serikali.

Pia, ameongeza kuwa hiyo ni fursa kwa taasisi za umma kujifunza, kubadilishana uzoefu na kuonesha mafanikio, ubunifu na maboresho yaliyofanyika katika utoaji wa huduma kwa umma.

Wananchi wanaotembelea banda la BoT wanapata fursa ya kujifunza masuala mbalimbali ikiwemo; Uwekezaji katika hatifungani, alama za usalama katika noti, majukumu ya BoT, namna ya kupata leseni ya kutoa huduma ndogo za fedha, mfumo wa malipo wa Tanzania unavyofanya kazi na nafasi ya BoT katika uchumi wa nchi.

Ushiriki wa BoT katika maonesho hayo ni sehemu ya mkakati wake wa kuendelea kuimarisha mawasiliano kwa umma, kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu shughuli zake na kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi.







# BoT YASHIRIKI MAONESHO YA KARIBU KILIFAIR

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeshiriki Maonesho ya Karibu Kilifair yaliyofanyika jijini Arusha na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu majukumu yake.

Maonesho hayo yaliyolenga kuhamasisha utalii yalianza Juni 4 na kuhitimishwa Juni 7, 2026 katika Viwanja vya Magereza jijini Arusha, yakishirikisha taasisi mbalimbali za umma na binafsi.

Katika maonesho hayo, BoT ilitoa elimu kuhusu namna ya kutambua alama za usalama zilizopo kwenye noti, utunzaji bora wa fedha ili zidumu kwa muda mrefu, pamoja na taratibu za kubadilisha noti zilizoharibika.

Akizungumza wakati wa maonesho hayo, Meneja wa Uendeshaji wa BoT Tawi la Arusha, Bw. Cretus Mwakalinga, alisema wananchi wengi bado hawana uelewa wa kutosha kuhusu haki yao ya kubadilisha fedha zilizoharibika na kupata thamani yake endapo zitakidhi vigezo vilivyowekwa.

"Miongoni mwa vigezo muhimu ni kwamba noti iliyoharibika inapaswa kubaki na angalau asilimia 75 ya umbo lake la awali ili iweze kubadilishwa na kupata thamani yake kamili," alisema Bw. Mwakalinga.

Ushiriki wa BoT katika maonesho hayo ni sehemu ya mkakati wa kuwafikia wananchi katika maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuimarisha uelewa kuhusu majukumu yake na huduma zinazotolewa kwa umma.





# GAVANA TUTUBA AONGOZA KIKAO CHA 18 CHA BARAZA LA HUDUMA JUMUISHI ZA FEDHA



Gavana Emmanuel Tutuba akizungumza katika kikao cha 18 cha Baraza la Taifa la Huduma Jumuishi za Fedha kilichofanyika tarehe 20 Mei 2026 jijini Dodoma.

Baraza la Taifa la Huduma Jumuishi za Fedha, likiongozwa na Mwenyekiti wake ambaye pia ni Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Emmanuel Tutuba, limefanya kikao chake cha 18 , tarehe 20 Mei 2026, katika ofisi za BoT jijini Dodoma.

Baraza hilo, lenye wajumbe 29 kutoka serikalini na sekta binafsi, limejadili mikakati mbalimbali inayolenga kuimarisha upatikanaji na matumizi ya huduma rasmi za fedha kwa wananchi, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kukuza ujumuishaji wa kifedha nchini.



Mwenyekiti wa Umoja wa Kampuni za Simu Tanzania (TAMNOA) ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom, Bw. Philip Besiimire, akielezea jambo katika kikao cha 18 cha Baraza la Taifa la Huduma Jumuishi za Fedha kilichofanyika tarehe 20 Mei 2026 jijini Dodoma.



Mkurugenzi wa Umoja wa Mabenki Tanzania, Bi. Tuse Joune, akifafanua jambo katika kikao cha 18 cha Baraza la Taifa la Huduma Jumuishi za Fedha kilichofanyika tarehe 20 Mei 2026 jijini Dodoma.



Gavana Emmanuel Tutuba akizungumza katika kikao cha 18 cha Baraza la Taifa la Huduma Jumuishi za Fedha kilichofanyika tarehe 20 Mei 2026 jijini Dodoma.

# BOT NA HESLB KUIMARISHA ELIMU YA FEDHA KWA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU




Gavana Emmanuel Tutuba pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia baada ya uzinduzi wa utekelezaji wa hati ya makubaliano kati ya BoT na HESLB iliyofanyika BoT jijini Dodoma tarehe 18 Mei 2026.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa kushirikiana na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imezindua rasmi utekelezaji wa hati ya makubaliano yenye lengo la kuimarisha elimu ya fedha kwa wanafunzi wa elimu ya juu nchini.

Akizungumza katika hafla hiyo iliyofanyika tarehe 18 Mei 2026 katika ofisi za BoT jijini Dodoma, Gavana wa BoT, Bw.Emmanuel Tutuba, alisema kuwa hatua hiyo ni sehemu ya juhudi za pamoja za kuwawezesha vijana wa Kitanzania kwa kuwapatia maarifa ya kifedha na stadi muhimu za usimamizi wa fedha.

Alieleza kuwa kupitia ushirikiano huo, wanafunzi watanufaika na programu maalum ya elimu ya fedha itakayopatikana kupitia mfumo wa akaunti binafsi ya mwanafunzi unaojulikana kama Students' Individual Permanent Account (SIPA). Mfumo huo utarahisisha upatikanaji wa elimu ya fedha kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu kote nchini kupitia majukwaa ya kidijitali.

Gavana Tutuba alibainisha kuwa programu hiyo itajikita katika maeneo muhimu ikiwemo uandaaji wa bajeti, uwekaji wa akiba, matumizi sahihi ya mikopo, mipango ya kifedha, matumizi ya huduma za kifedha kidijitali, pamoja na ulinzi wa mtumiaji wa huduma za fedha.

Aliongeza kuwa maarifa hayo yatawasaidia wanafunzi na wahitimu kuwa na nidhamu ya kifedha, kufanya maamuzi sahihi ya kifedha, na hatimaye kuchangia kwa ufanisi katika maendeleo ya uchumi wa taifa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia, alieleza kuwa taasisi hiyo inatambua wajibu wake mkubwa katika kuhakikisha utekelezaji wa makubaliano hayo unakuwa wenye tija na mafanikio.

Aidha, alibainisha kuwa HESLB itashirikiana na BoT katika kupitia, kuboresha na kupakia maudhui hayo ili kuhakikisha yanakuwa sahihi, bora na yenye manufaa kwa wanafunzi. Pia, taasisi hiyo itaweka mfumo madhubuti wa ufuatiliaji na tathmini utakaosaidia kupima ufanisi wa programu hiyo na kufanya maboresho pale inapobidi.

Uzinduzi huo unaashiria hatua muhimu katika kuimarisha ujumuishaji wa kifedha na kuwajengea vijana msingi imara wa ustawi wa kifedha, sambamba na kukuza uchumi endelevu wa Tanzania.



Gavana Emmanuel Tutuba akifafanua jambo katika hafla ya uzinduzi wa utekelezaji wa hati ya makubaliano kati ya BoT na HESLB iliyofanyika BoT jijini Dodoma tarehe 18 Mei 2026.

# MABADILIKO YA KIDIJITALI YANAVYOONGEZA UFANISI BoT



Katika kipindi ambacho mageuzi ya kidijitali yanaendelea kushika kasi duniani, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeendelea kuimarisha matumizi ya teknolojia za kisasa ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli zake.

Mageuzi ya teknolojia ya kidijitali yameendelea kuibadilisha BoT kwa kasi kubwa, huku yakiongeza ufanisi wa kazi, kupunguza gharama za uendeshaji na kuboresha huduma kwa wananchi.

Katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni, BoT imewekeza katika mifumo ya kisasa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) ambayo inarahisisha utendaji wa kazi zake na kuongeza ufanisi.

Yafuatayo ni mafanikio yaliyopatikana kutokana na BoT kuanza kutumia mifumo hiyo ya kidijiti katika ufanyaji wake wa kazi.

**Mfumo wa malipo wenye kasi zaidi**
Kurugenzi ya Huduma za Kibenki ni moja ya maeneo yaliyonufaika zaidi na mageuzi hayo, akizungumzia mafanikio hayo, Mkurugenzi wa Kurugenzi hiyo, Bw. Agathon Kipandula anasema matumizi ya mifumo ya kidijitali yameongeza uzalishaji na tija.

"Mwaka 2010 tulikuwa tunashughulikia miamala 2,000 kwa siku kwa kutumia wafanyakazi 60. Mwaka 2026 tunashughulikia zaidi ya miamala 5,000 kwa siku kwa wafanyakazi 32 pekee," anasema.

Anasema hayo yote ni mafanikio ya kuanza kutumika kikamilifu kwa mifumo hiyo ya kidijitali, pia ameongeza kuwa matumizi ya hundi yamepungua kwa kiasi kikubwa na hivyo kupunguza gharama za uchapishaji wa nyaraka nyeti.

**Teknolojia katika usimamizi wa sarafu**
Kwa upande wa Kurugenzi ya Usimamizi wa Sarafu, teknolojia imeongeza uwezo wa kufanya makadirio sahihi ya fedha zinazohitajika nchini pamoja na kuboresha usalama wa noti na sarafu. Kurugenzi hiyo inaeleza kuwa mifumo ya kidijitali imesaidia kupata takwimu sahihi za matumizi ya fedha na kusaidia kufanya maamuzi ya kisera.
"Teknolojia imetusaidia kuongeza ufanisi katika usimamizi wa fedha na utoaji wa elimu kwa wananchi kupitia majukwaa ya kidijitali," anasema Ngulimi Balele ambaye ni Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Usimamizi wa Usimamizi wa Sarafu.

**Kasi ya uchambuzi wa takwimu**
Miongoni mwa majukumu ya BoT ni utafiti wa uchumi na uchambuzi wa taarifa zinazopatikana. Matumizi ya mifumo ya kidijitali inatajwa kuongeza kasi ya uchambuzi wa taarifa za uchumi.
Akizungumzia suala hiyo, Mkurugenzi wa Tafiti na Sera za Uchumi Dkt. Suleiman Missango, anasema matumizi ya takwimu kubwa (Big Data) yanaisaidia Benki Kuu kufanya maamuzi ya haraka na sahihi.

"Mifumo ya kidijitali imerahisisha ukusanyaji wa takwimu na uchambuzi wa taarifa za uchumi kwa wakati," anasema Dkt. Missango.

**Elimu ya fedha kupitia majukwaa ya kidijitali**
Katika kuwafikia jamii kwa ujumla kuhusu majukumu ya BoT pamoja na elimu ya fedha ili kukuza uchumi jumuishi, mitandao ya kijamii inatumika zaidi katika kuwafikia watu wengi.

Mkurugenzi anayesimamia Ustawi na Huduma Jumuishi za Fedha, Bw. Kennedy Komba anasema kupitia mifumo ya kidijitali, wananchi sasa wanaweza kupata elimu ya fedha, kuwasilisha malalamiko na kupata huduma mbalimbali kwa urahisi.

Bw. Komba anasema mfumo wa SEMA na BOT umeongeza uwazi na ufanisi katika kushughulikia malalamiko ya wananchi kidijitali.

"Wananchi sasa wanaweza kuwasilisha malalamiko yao kwa njia ya simu au tovuti bila kufika Benki Kuu," anasema Bw. Komba.

Aidha, matumizi ya mitandao ya kijamii na majukwaa ya mtandaoni yamepanua wigo wa utoaji elimu ya fedha kwa vijana, wanawake na wafanyabiashara.

**AI na usimamizi wa sekta ya fedha**
Kurugenzi ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha nayo imeanza kutumia mifumo ya kisasa ya kidijitali katika usimamizi wa benki na taasisi za fedha.

Mkurugenzi wa Kurugenzi hiyo anasema Benki Kuu inaendelea kujenga mfumo wa usimamizi wa papo hapo (Real-Time Supervision System) utakaowezesha usimamizi wa karibu na wenye ufanisi.

"Tunajenga mfumo wa kisasa utakaotumia teknolojia za Akili Unde (AI) hatua ambayo itasaidia kutambua vihatarishi mapema na kusaidia kuifanya sekta ya fedha kuwa thabiti," anasema Sadati Musa ambaye ni mkurugenzi katika eneo hilo.

**Usalama wa mifumo ya malipo**
Kurugenzi ya Mifumo ya Malipo ya Taifa imekuwa mhimili mkuu wa mageuzi ya malipo ya kidijitali Benki Kuu pamoja na nchi kwa ujumla.

Kupitia mifumo ya TISS, TACH na TIPS, wananchi wanaweza kufanya miamala ya papo kwa papo ndani ya saa 24. Mkurugenzi wa Kurugenzi hiyo, Bi. Lucy Shahidi anasema mifumo hiyo imechochea kwa kiasi kikubwa uchumi usiotegemea fedha taslimu.

"TIPS imeunganisha benki na mitandao ya simu na hivyo kuondoa vikwazo vya miamala baina ya watoa huduma, Benki Kuu pia imeendelea kupunguza gharama za miamala ya kidijitali ili wananchi wengi zaidi waweze kutumia huduma hizo,"anasema Bi. Lucy.

Bi. Lucy anaongeza kuwa mageuzi ya kidijitali yameifanya Benki Kuu kuwa taasisi yenye ufanisi mkubwa zaidi na usalama wa uhakika katika mifumo ya malipo.

Aidha, Gavan awa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba akizungumzia mifumo ya malipo na maendeleo ya kidijitali nchini akichangia katika mjadala wa mawaziri wakati wa Kikao cha 58 cha Tume ya Uchumi ya Afrika (ECA), kinachofanyika jijini Tangier, Morocco, Machi 28, 2026 alisema;

"Tanzania imepiga hatua kubwa katika ujumuishaji wa kifedha kupitia huduma za fedha kwa njia ya simu na mifumo ya malipo yakidigitali yenye ufanisi, mafanikio hayo yamechangia kupunguza gharama za miamala, kurahisisha ukusanyaji wa mapato ya serikali na kuongeza uwazi katika matumizi ya fedha,"alisema Bw. Tutuba.

Bw. Tutuba aliongeza kuwa Tanzania ni sehemu ya mifumo ya malipo ya kikanda ikiwemo Mfumo wa Malipo wa Afrika Mashariki (EAPS) na Mfumo wa Malipo wa Ukanda wa Kusini mwa Afrika (SADC RTGS). Vilevile, amebainisha kuwa benki za biashara nchini zinaendelea kujiunga na Mfumo wa Malipo wa Afrika (PAPSS), unaowezesha miamala ya kifedha kati ya nchi za Afrika kwa haraka na ufanisi, hatua itakayochochea biashara na kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi barani Afrika.

# MIAKA SITINI BOT, KWA UCHUMI ENDELEVU

1. *Moja tisa sita sita, Benki Kuu kuingia,*
   *Gavana tukampata, hapa kwetu Tanzania,*
   *Kazi anza ichakata, kulenga Watanzania,*
   *Miaka sitini BoT, kwa uchumi endelevu.*

2. *Majukumu kwa malengo, yale tulijipatia,*
   *Kuendana na mipango, Taifa kusaidia,*
   *Ikaufanya mchango, ule unaovutia,*
   *Miaka sitini BoT, kwa uchumi endelevu.*

3. *Kutoka uchumi hodhi, dola ikitupangia,*
   *Hadi kufikia hadhi, soko kutuamulia,*
   *Bila ya kuomba radhi, malengo tumefikia,*
   *Miaka sitini BoT, kwa uchumi endelevu.*

4. *Changamoto zimepita, nchi zilizotishia,*
   *Walakini tumepeta, kwa kuzihimili pia,*
   *Uchumi haujagota, nchi yetu Tanzania,*
   *Miaka sitini BoT, kwa uchumi endelevu.*

5. *Tuna uchumi huria, wengi ukiwavutia,*
   *Benki Kuu Tanzania, vema tunasimamia,*
   *Kanuni za kutumia, mabenki twayapatia,*
   *Miaka sitini BoT, kwa uchumi endelevu.*

6. *Kudhibiti mfumuko, ni sera ya fedha pia,*
   *Lengo kuu la mashiko, hapa kwetu Tanzania,*
   *Na mafanikio yako, kweli tunajivunia,*
   *Miaka sitini BoT, kwa uchumi endelevu.*

7. *Sekta yetu ya mabenki, vema twaisimamia,*
   *Kazi zake zinatiki, hata ukiangalia,*
   *Tunazo benki lukuki, umma zauhudumia,*
   *Miaka sitini BoT, kwa uchumi endelevu.*

8. *Mifumo malipo pia, tuko juu Tanzania,*
   *Kwa tunavyoitumia, kwetu waja jifunzia,*
   *Huduma twajipatia, kwa haraka sana pia,*
   *Miaka sitini BoT, kwa uchumi endelevu.*

9. *Yaweza uhimilivu, Benki Kuu Tanzania,*
   *Imekuwa ni shupavu, changamoto kitujia,*
   *Viongozi ni wa nguvu, na wafanyakazi pia,*
   *Miaka sitini BoT, kwa uchumi endelevu.*

10. *Sasa tunasonga mbele, Benki Kuu Tanzania,*
    *Majukumu ya milele, vema tukisimamia,*
    *Kwa bidii na uwazi, kupaisha Tanzania,*
    *Miaka sitini BoT, kwa uchumi endelevu.*

11. *Changamoto bado nyingi, katika yetu dunia,*
    *Ila jambo la msingi, mipango imetulia,*
    *Kuzidi upiga mwingi, uchumi kusimamia,*
    *Miaka sitini BoT, kwa uchumi endelevu.*

12. *Hongera kwa Benki Kuu, sitini imetimia,*
    *Hebu zidi kwenda juu, hudumia Tanzania,*
    *Wananchi wawe juu, uchumi ukivutia,*
    *Miaka sitini BoT, kwa uchumi endelevu.*

13. *Uchumi uwe thabiti, na uwekezaji pia,*
    *Tena hizi zetu noti, ambazo tunatumia,*
    *Vizuri tujizatiti, kidijiti kutumia,*
    *Miaka sitini BoT, kwa uchumi endelevu.*

***Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)***

**Limetolewa na Idara ya Mawasiliano**
**Benki Kuu ya Tanzania**

---

Anuani:
**Barabara ya 16 ya Jakaya Kikwete, 40184**
**S.L.P. 2303 Dodoma, Tanzania**
Barua pepe:
**botcommunications@bot.go.tz**
**info@bot.go.tz**
Tovuti:
**www.bot.go.tz**